## YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI ........ - 1 -

1.1. MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA ILANI KWA KILA SEKTA ........ - 1 -

1.2. HITIMISHO ........ - 3 -

2.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI MBALIMBALI KIKATA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2015-2020 ........ - 3 -

2.1. KATA YA RUTUNGURU ........ - 3 -

2.2. KATA YA KIBINGO ........ - 1 -

2.3. KATA YA MURONGO ........ - 2 -

2.4. KATA YA BUGOMORA ........ - 6 -

2.5. KATA YA KIBARE ........ - 7 -

2.6. KATA YA KYERWA ........ - 9 -

2.7. KATA RUKURAIJO ........ - 5 -

2.8. KATA ISINGIRO ........ - 9 -

2.9. KATA KAISHO ........ - 12 -

2.10. KATA NYARUZUMBURA ........ - 15 -

2.11. KATA KIKUKURU. ........ - 16 -

2.12. KATA YA NYAKATUNTU ........ - 18 -

2.13. KATA YA KAKANJA ........ - 19 -

2.14. KATA YA KIMULI ........ - 21 -

2.15. KATA YA RWABWERE ........ - 22 -

2.16. KATA YA SONGAMBELE ........ - 24 -

2.17. KATA YA KITWECHENKURA ........ - 27 -

2.18. KATA YA NKWENDA ........ - 1 -

2.19.KATA YA ITEERA ........................................................................................................ - 4 -

2.20.KATA YA MABIRA........................................................................................................ - 7 -

2.21.KATA YA KITWE ........................................................................................................ - 11 -

2.22.KATA YA KAMULI ........................................................................................................ - 12 -

2.23.KATA YA BUGARA ........................................................................................................ - 14 -

2.24.KATA YA BUSINDE........................................................................................................ - 15 -

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI 2015-2020 HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA

## 1.0 UTANGULIZI

Katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa imetekeleza miradi mingi ya maendeleo. Lengo la utekelezaji wa miradi hiyo ni kuhakikisha Serikali inafikisha huduma stahiki kwa wananchi wake.

Aidha, kuanzia mwaka 2015-2020, kipindi cha miaka 5 ya Utawala wa Chama Cha Mapinduzi, Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa imetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika kila kata ikikusudia wananchi wapate huduma za jamii zinazokidhi mahitaji yao.

## 1.1. MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA ILANI KWA KILA SEKTA

***1.1.1. Afya:*** Katika kuboresha huduma za Afya Serikali imetumia zaidi ya Shilingi Bilioni 3.5 katika sekta hii. Serikali imewezesha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kwa gharama ya Shilingi 1,800,000,000. Mradi huu umekamilika kwa baadhi ya miundombinu muhimu na umeanza kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa wa nje (OPD). Vilevile, Shilingi 1,100,000,000 zilitolewa na Serikali kwa ajili ya kuboresha Vituo vya Afya vya Murongo na Kamuli pamoja na kununua vifaa tiba ambavyo vinatumika kutolea huduma katika vifaa hivyo. Sambamba na hilo, Serikali imeboresha miundombinu ya vituo vyote vya kutolea huduma za afya Wilayani Kyerwa kwa kufanya ukarabati.

***1.1.2. Elimu:*** Katika kuhakikisha mazingira ya kutolea huduma ya elimu Serikali imetumia zaidi ya bilioni 2.3 kutekeleza miradi mbalimbali ya sekta ya elimu. Hii ni pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa Maabara za sayansi katika Shule za Sekondari 21 ambazo zimekamilika na zinatoa huduma iliyokusudiwa. Pia ujenzi wa vyumba vya madarasa 78 kwa shule za Msingi 53 na vyumba vya madarasa 43 kwa Shule za Sekondari 14. Hii ni sambamba na ukamilishaji wa maboma 8 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi pamoja na ujenzi wa matundu ya vyoo 475 katika Shule za Msingi na 40 katika Shule za Sekondari.

***1.1.3. Maji:*** Kwa kutambua umuhimu wa maji katika maisha, Serikali imewezesha ujenzi na uboreshaji wa miradi 26 ya maji ndani ya Wilaya yenye thamani ya bilioni 7.5. Hii ni pamoja na miradi ya Kigorogoro, Iteera, Rwabikagate. Aidha miradi ya Mabira, imefanyiwa ukarabati na inatoa huduma. Mradi mkubwa wa maji utakaonufaisha Vijiji 57 unaoendelea na utekelezaji na unatarajia kukamilika kabla ya mwaka 2020 kuisha.

***1.1.4. Barabara*:** Serikali imeendele kuboresha miundombinu ya barabara wilayani Kyerwa kwa kujenga maeneo korofi ya barabara katika viwango vya lami, kufanya matengenezo ya kawaida, kujenga makalvati na matengenezo ya muda maalumu. Kwa kipindi cha miaka 5

Serikali imejenga barabara zenye urefu wa Km.1,848.25 na makalvati 176 kwa gharama ya zaidi ya Bilioni 7 .Pia ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika maeneo ya Kata ya Rutunguru, Nkwenda na Kyerwa, Wananchi wanaendelea kunufaika na miundombinu hiyo.

***1.1.5. Umeme:*** Katika Wilaya ya Kyerwa Serikali imefanikiwa kufikisha miundombinu ya umeme katika Vijiji 66 kati ya 99 na vitongoji 164 na kuhakikisha Wananchi wananufaika na umeme huo katika kufanya shughuli za maendeleo. Aidha, upanuzi wa miundombinu ya umeme kuelekea maeneo ambayo hayakufikiwa unaendele kupitia REA awamu ya tatu.

***1.1.6. Utawala:*** Serikali imewezesha ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Halmashauri katika eneo la mji wa Rubwera kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwa Wananchi, ujenzi umefikia hatua ya kumwaga jamvi la ghorofa ya pili. Aidha Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya lipo katika hatua ya ukamilishaji, vilevile Ofisi za TANESCO Makao Makuu ya Wilaya zimekamilika na zinatoa huduma kwa wananchi.

***1.1.7. Kilimo na Ufugaji:*** Serikali imeendelea kutambua Sekta ya Kilimo kama Uti wa mgongo wa Nchi na hivyo kuendelea kuwekeza katika sekta hiyo. Vikundi 125 vya Kilimo na Ufugaji vimewezeshwa kwa gharama ya Shilingi 70,000,000.00 katika kipindi cha miaka 5 ili kuendeleza sekta ya Kilimo na kuendelea kunufaisha Wananchi. Aidha mashamba darasa ya mazao muhimu kama kahawa na migomba yameanzishwa kwa lengo la kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa mbegu bora ya mazao hayo hatimaye kuongeza uzalishaji. Uzalishaji wa ndizi umeongezeka kutoka tani 186,937 kwa mwaka 2015 hadi 419,247 kwa mwaka 2020. Aidha uzalishaji wa zao la kahawa umeongezeka kutoka tani 22,620 kwa mwaka 2015 hadi tani 29,994 kwa mwaka 2020.

Aidha Serikali imewezesha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo hususani ng’ombe kwa ajili ya kuboresha koosafu za ng’ombe ili kuongeza uzalishaji wa mifugo na mazao yake. Katika kipindi hiki jumla ya ng’ombe 452 wamehimilishwa kwa ajili ya kuboresha koosafu kwa kutumia mbegu za madume bora. Elimu kwa wafugaji juu ya uzalishai bora wa mifugo imetolewa kupitia vikundi 24 ma mikutano ya wafugaji. Pia Serikali imewezesha ukarabati wa miundombinu ya mifugo yakiwemo majosho yanayotumika katika udhibiti wa magonjwa ya mifugo.

***1.1.8. TASAF:*** Katika kuendelea kuboresha maisha ya Wananchi kutoka kaya masikini sana Serikali imetumia jumla ya Bilioni 7.9 zilizonufaisha kaya 9,391 masikini katika vijiji 54 tangu mwaka 2015 mpaka 2020 katika kusaidia kaya masikini sana ili ziweze kujikimu kimaisha. Pia utambuzi wa kaya ambazo hazikuingizwa kwenye mpango na maeneo ya utawala ambayo hayakuingizwa, mpango unaendelea ili kuhakikisha kila kaya masikini sana inanufaika kupitia mfuko wa Tasaf.

***1.1.9. Ardhi na Maliasili***: serikali imewekeza zaidi ya kiasi cha Shilingi 53,000,000.00 katika sekta hii ili kuhakikisha upimaji wa viwanja 323 katika Halmashauri ya Wilaya Kyerwa, utolewaji wa hati miliki 364 kwa viwanja vilivyopimwa, upandaji miti 80,000 katika shule za msingi na sekondari pamoja na uwekezaji katika Misitu. Aidha, serikali imesimamia upandaji wa miti 80,000 kwa gharama ya Shilingi 16,000,000.00, katia shule za Msingi za Kyerwa, Anza Kuelimisha, Kaina, Ishaka, Kibimba, Rukuraijo; Shule za Sekondari za Isingiro, Kyerwa, Ibanda na Kitwechenkura.

***1.1.10. Mikopo ya Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu:-*** Katika kuhakikisha wananchi wa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu wanajikwamua kiuchumi Serikali imeendelea kutoa mikopo kwa ajili ya kuwezesha vikundi vya makundi hayo. Kwa kipindi cha miaka 5, jumla ya Shilingi 295,000,000 zimetolewa kwa ajili ya mikopo kwa lengo la kuinua ajira, kujitegemea na uchumi wao kwa ujumla. Vikundi 20 vya Vijana, 33 vya Wanawake na 9 vya Watu wenye Ulemavu vimewezeshwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za ujasiriamali.

## 1.2. HITIMISHO

Serikali ya awamu ya tano (5) imetumia ya Shilingi bilioni 34 katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miaka 5 wilayani Kyerwa. Fedha hizi zimetekeleza miradi iliyokamilika na inayoendelea kutekelezwa katika kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa Wananchi.

# 2.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI MBALIMBALI KIKATA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2015-2020

## 2.1. KATA YA RUTUNGURU

Katika Kata ya Rutunguru Serikali imetekeleza miradi 5 yenye thamani ya Shilingi **315,362,766.00**. Katika miradi hiyo 5 imekamilika na inatoa huduma na 1 unaendelea kutekelezwa. Ufafanuzi wa kila Mradi ni kama ifuatavyo:-

### *2.1.1.* Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na matundu 8 ya vyoo S/M Kilela

Kwa lengo la kuboresha na kupunguza changamoto za miundombinu katika sekta ya Elimu, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imejenga vyumba 2 vya madarasa na matundu 8 ya vyoo katika Shule ya Msingi Kilela. Mradi huu uligharimu jumla ya Shilingi 61,432,566.00 mpaka kukamilika na kuanza kutumika. Lengo la mradi ni kuimarisha miundombinu baada ya athari za tetemeko la Ardhi lililotokea Setpemba 10, 2016.



***Picha 1: Vyumba vya Madarasa S/M Kilela kwa ufadhili wa AfDB***



***Picha 2: Matundu 8 ya vyoo S/M Kilela kwa ufadhili wa AfDB***

Mradi huu umekamilika na ulianza kutumika mwaka 2018 na unahudumia wanafunzi zaidi ya 150

### 2.1.2 Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa S/M Nyakakoni

Mradi huu ni miongoni mwa miradi iliyofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa lengo la kupunguza athari za tetemeko la Ardhi lililotokea Mkoa wa Kagera mwaka 2016.

Mradi huu umegharimu jumla ya Shilingi 39,019,200.00. Mradi umekamilika na ulianza kutumika mwaka 2018.



**Picha 3: Vyumba viwili vya madarasa Shule ya Msingi Nyakakoni**

### 2.1.3. Ujenzi wa zahanati ya Rwensheshe

Katika kuhakikisha huduma bora za Afya kwa wananchi, Serikali imeanzisha mradi wa ujenzi wa zahanati katika Kijiji cha Rwensheshe ili Wananchi wa Kijiji hicho na Vijiji jirani waweze kunufaika kwa kupata huduma za afya zenye uhakika





*Picha 4: Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Rwensheshe*

Mradi huu umekadiriwa kugharimu kiasi cha zaidi ya Shilingi 200,000,000 mpaka kukamilika na mpaka hapo ulipofikia umegharimu kiasi cha Shilingi 9,500,000. Mradi unatarajia kuhudumia Wananchi wa Vijiji vya Rwensinga, Rwensheshe na Nyakakoni.

### 2.1.4. Ujenzi wa kipande cha barabara Rutunguru kwa kiwango cha lami

Serikali imejenga kipande cha barabara kwa kiwango cha lami katika Kijiji cha Rutunguru ili kuboresha miundombinu ya usafirishaji wilayani Kyerwa.



*Picha 5: Ujenzi wa kipande cha lami katika kijiji cha Rutunguru*

### 2.1.5. Miradi mingine katika Kata ya Rutunguru

miradi mingine iliyotekelezwa katika Kata ya Rutunguru ni pamoja na ujenzi wa matundu 4 ya vyoo S/M Rwensinga kwa gharama ya Shilingi 3,411,000.00, ujenzi wa mradi wa maji ya bomba ambao utekelezaji wake unaendelea, pamoja na uwezeshaji wa vikundi vya kijamii kikiwemo kikundi cha ufugaji wa kuku Tegemeo Kilela kilichowezeshwa na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani, FAO pamoja na fedha ya Mfuko wa Jimbo Shilingi 950,000.

## 2.2. KATA YA KIBINGO

Kata ya Kibingo ni moja ya maeneo ambayo miradi mbalimbali imetekelezwa wakati wa utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha mapinduzi.2015-2020. Miradi 3 imetekelezwa kwa thamani ya Shilingi **255,300,000.00**. Mchanganuo wa miradi ni kama ifuatavyo:-

### 2.2.1. Ujenzi wa nyumba ya Walimu (Two in one)na chumba cha darasa Shule ya Sekondari Ibanda

Ujenzi wa nyumba ya Walimu (Two in one) katika Shule ya Sekondari ya Ibanda ambao umekisiwa kugharimu Shilingi 35,000,000.00 pindi utakapokuwa umekamilika. Utekelezaji wa mradi unaendelea.



***Picha 6: Ujenzi wa nyumba ya Walimu (2 in 1) Shule ya Sekondari Ibanda- Kibingo***

### 2.2.2. Ukarabati wa Tanki la maji Shule ya Msingi Rugasha

Serikali imefanya ukarabati wa tanki la maji katika Shule ya Msingi Rugasha kwa gharama ya Shilingi 300,000 mwaka 2016/17 kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama shuleni hapo kwa matumizi ya wanafunzi na walimu.

### *2.2.3.* Ujenzi wa mradi wa maji katika Kijiji cha Kibingo

Ujenzi wa miundombinu ya maji katika Kijiji cha Kibingo kupitia Wakala wa Maji (RUWASA) unaendelea ili kuhakikisha Wananchi wanapata uhakika wa maji safi na salama.

## 2.3. KATA YA MURONGO

Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa lengo la kuhakikisha eneo la mpaka wa Murongo linakuwa na huduma bora za kijamii. Kwa kipindi cha miaka 5, jumla ya miradi 10 yenye thamani ya Shilingi **2,117,313,783.90** imetekelezwa Kata ya Murongo. Mchanganuo wa miradi ni kama ifuatavyo:-

### 2.3.1. Ujenzi wa Kituo cha Afya Murongo

Ili kuimarisha utoaji huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya, serikali imetekeleza ujenzi wa majengo 5 mapya katika Kituo cha Afya Murongo kwa gharama ya Shilingi 400,000,000. Fedha hizi ziliwezesha ujenzi wa wodi ya wazazi, maabara, chumba cha upasuaji, chumba cha kuhifadhia maiti na nyumba ya Mganga.

Mradi huu ulianza kutekelezwa mwaka 2018 na kukamilika 2019 na kwa sasa majengo yanatumika kwa kutoa huduma kwa Wananchi. Pia Serikali ilitoa kiasi cha Shilingi 300,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika Kituo cha Afya Murongo ambavyo vinatumika katika utoaji huduma.



***Picha 7: Chumba cha upasuaji Kituo cha Afya Murongo***



***Picha 8: Wodi ya Wazazi Kituo cha Afya Murongo***

### 2.3.2. Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa, matundu 8 ya vyoo na nyumba ya walimu S/M Omukachili

Kupitia Mfuko wa Maafa Mkoa, Benki ya Maendeleo Afrika iliwezesha ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa, nyumba ya walimu (2 in 1) na matundu 8 ya vyoo Shule ya Msingi Omukachili. Mradi huu uligharimu jumla ya Shilingi 162,750,000. Aidha vyumba 2 vya madarasa, ofisi ya Mwalimu mkuu na nyumba 1 ya mwalimu vilijengwa katika shule hii kwa gharama ya Shilingi 65,050,500 kwa fedha zilizotolewa na Mfuko wa Maafa Mkoa.


*Picha 9: nyumba ya Mwalimu S/M Omukachili*


*Picha 10: Vyumba 3 vya madarasa S/M Omukachili*

### 2.3.3. Ukamilishaji wa vyumba vya maabara Shule ya Sekondari Murongo

Katika kuhakikisha wanafunzi wanasomea mazingira rafiki serikali ilifanya ukamilishaji wa maabara za masomo ya sayansi katika shule ya sekondari Murongo kwa gharama ya Shilingi 17,150,870 kutoka mfuko wa EP4R.

### 2.3.4. Ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu 4 ya vyoo Shule ya Msingi Murongo

Vyumba vya madarasa 3 na matundu 4 ya vyoo yamejengwa katika shule ya msingi Murongo kwa kushirikiana na Kampuni inayojenga umeme ya Kikagati Hidroelectric Power kwa gharama ya Shilingi 100,000,000.

### *2.3.5.* Ujenzi wa nyumba ya Mwalimu

Ujenzi wa nyumba ya walimu kwa gharama ya Shilingi 60,000,000 kwa nguvu za wananchi shule ya msingi Murongo umekamilika na unatumika.

### 2.3.6. UJENZI wa vyumba 3 vya madarasa Shule ya Msingi Masheshe

Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa Shule ya Msingi Masheshe umegharimu jumla ya Shilingi 74,491,800.00 kwa ufadhili wa Serikali ya Afrika Kusini kupitia Shirika la Maendeleo Duniani, UNDP, vyumba vimekamilika.



***Picha 11: Vyumba 3 vya madarasa Shule ya Msingi Murongo***

### 2.3.7. Ukamilishaji wa ofisi ya Kata ya Murongo

Katika kipindi cha miaka 5 (2015-2020), serikali imekamilisha ujenzi wa ofisi ya kata Murongo iliyokwama kwa muda mrefu. Ukamilishaji huo uligharimu jumla ya Shilingi 17,374,375.00 fedha za Halmashauri na ofisi ilianza kutumika tangu mwaka 2017.



***Picha 12: Ofisi ya Kata ya Murongo***

### 2.3.8. Ujenzi wa Ofisi ya Kijiji Murongo

Vilevile, Serikali imejenga Ofisi ya Kijiji cha Murongo kwa gharama ya Shilingi 39,700,000 kwa fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ya Kijiji, mradi umekamilika na ulianza kutumika tangu mwaka 2017.

### *2.3.*9. Ujenzi wa mradi wa maji Rwabikagate

Serikali imetekeleza ujenzi wa mradi mkubwa wa maji Rwabikagate kwa gharama ya Shilingi 880,796,238.88 ambao unatoa huduma ya maji katika kijiji cha Rwabikagate na vijiji jirani.

### *2.3.10.* Miradi mingine Kata ya Murongo

Pamoja na shughuli hizo katika Kata ya Murongo serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa bweni shule ya sekondari Murongo, ujenzi wa matundu ya vyoo shule ya msingi Murongo, ukarabati wa barabara za Amsheshe-Kituo cha Afya Murongo, Murongo ferry- Ibanda, Rwabikagate Oumukachili, Rwabikagate-Wichila pamoja na ujenzi wa makalvati na ufadhili wa vikundi 5 vya Wanawake na 6 vya Vijana.

## 2.4. KATA YA BUGOMORA

Katika utekelezaji wa ilani ya Chama Tawala, Kata ya Bugomora imetekeleza miradi 5 ya maendeleo yenye thamani ya Shilingi **257,968,300.00** katika kipndi cha miaka 5. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

### 2.4.1. Ujenzi wa matundu ya vyoo

Ujenzi wa matundu 52 ya vyoo katika shule za Msingi za Magoma (12), kagu (8), Nyamiyaga (16) na nyakatera (16). Mradi huu ulianza mwaka 2015 na umekamilika mnamo mwaka 2020 kwa gharama ya Shilingi 43,773,500.00 na vyoo vinatumika

### 2.4.2. Ujenzi wa vyumba 6 vya madarasa Shule za Msingi Nyamiyaga, Kagu na Magoma

Ujenzi wa vyumba 6 vya madarasa katika Shule za Msingi za Nyamiyaga (3), Kagu 1 na Magoma S/M (2) kwa gharama ya Shilingi 86,980,000.00, madarasa hayo yamekamilika mwaka 2020. Wanafunzi zaidi ya 240 wananufaika na matumizi ya vyumba hivi vya madarasa

### 2.4.3. Ujenzi wa nyumba 3 za Walimu Shule za Msingi Magoma na Kagu

Ukamilishaji wa nyumba 3 za walimu Shule za Msingi za Magoma na Kagu. Kati ya hizo, nyumba 2 zimekamilika na zinatumika na moja inaendelea kujengwa ipo usawa wa linta. Gharama za ukamilishaji wa nyumba hizi ni Shilingi 31,000,000 kwa nguvu za Wananchi. Nyumba zilizokamilika zinatumiwa na walimu 4.

### 2.4.4. Ukarabati wa zahanati za Vijiji Nyakatera na Kagu

Ukarabati wa vituo hivyo vya kutolea huduma za afya umefanyika kwa vipindi tofauti kwa gharama ya jumla ya Shilingi 4,370,000 kutoka mfuko wa RBF. Mradi unanuafaisha watumiaji zaidi ya 6,576.

### 2.4.5. Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa Shule ya Msingi Nyamiyaga

Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa S/M Nyamiyaga kwa ufadhili wa Serikali ya Afrika Kusini kupitia Shirika la Maendeleo Duniani, UNDP, yamekamilika. Mradi huu umegharimu Shilingi 74,491,800 na umejengwa kuanzia Septemba, 2019 na kukamilika Agosti, 2020.



***Picha 13: Vyumba vya madarasa Nyamiyaga kwa ufadhili wa UNDP***

## 2.5. KATA YA KIBARE

Katika kata ya Kibare Serikali imeweza kutekeleza miradi mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma stahiki. Miradi mikubwa 3 yenye thamani ya Shilingi **761,000,000.00** imetekelezwa katika Kata ya Kibare kwa mchnganuo ufuatao:-

### 2.5.1. Ujenzi wa madarasa Shule ya Msingi Kishanda

Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa Shule ya Msingi Kishanda umegharimu jumla ya Shilingi 13,000,000 (12,000,000 kutoka mfuko wa P4R, 1,000,000 mchango wa Halmashauri). Ukamilishaji wa vyumba hivyo bado unaendelea.



*Picha 14:Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa S/M Kishanda*

### 2.5.2. Ujenzi wa mradi wa maji Kigorogoro

Ujenzi wa mradi mkubwa maji wa Kigorogoro uligharimu zaidi ya Shilingi 650,000,000, fedha zilizotolewa na Serikali Kuu. Mradi huu umesambaza maji katika maeneo ya Kijiji cha Kigorogoro, Rulama, Kishanda na Kibare.



*Picha 15: Tanki la maji katika mradi wa maji Kigorogoro-Kibare*

### 2.5.3. Ujenzi wa Maabara Shule ya Sekondari Bogomora

Ujenzi wa Maabara 3 kwa ajili ya masomo ya sayansi (Baologia, Fizikia na Kemia) Shule ya Sekondari Bugomora, mradi ulikamilika mwaka 2017 kwa gharama ya zaidi Shilingi 98,000,000 ikiwa ni mchango wa Halmashauri na nguvu za Wananchi.

#### 2.5.4. Ujenzi wa vyumba vya madarasa Bugomora Sekondari

Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Bugomora kwa fedha toka Halmashauri na nguvu za Wananchi uko hatua za ukamilishaji na unatarajia kukamilika kabla ya kumalizika kwa mwaka 2020.

#### 2.5.5. Ukarabati wa zahanati za Vijiji Kibare na Kigorogoro

Serikali imewezesha fedha za ukarabati wa Zahanati za Kibare na Kigorogoro kupitia fedha za RBF na kuongeza baadhi ya miundombinu kwa lengo la kuboresha utoaji huduma za afya katika kata ya Kibare.

### 2.6. KATA YA KYERWA

Katika kuhakikisha utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya chama tawala, Serikali imeweza kutekeleza miradi 14 yenye thamani ya Shilingi **6,760,214,807.20** katika Kata ya Kyerwa katika sekta za Afya, Maji, Elimu, Umeme na Utawala. Miradi iliyotekelezwa katika Kata ya Kyerwa ni kama ifuatavyo:-

#### 2.6.1. Ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri katika eneo la Rubwera, Makao Makuu ya Wilaya

2. Mradi huu ulianza kutekelezwa mwaka 2017 kupitia fedha za Serikali Kuu. Jengo limefikia ghorofa ya 2 na gharama iliyotumika mpaka kufikia hapo ni Shilingi 1,900,000,000 zilizotolewa na Serikali Kuu kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI. Jengo limekisiwa kutumia jumla ya Shilingi 5,000,000,000 mpaka kukamilika kwake.



***Picha 16: Jengo linalojengwa la Ofisi za Makao Makuu ya Halmashauri***

### 2.6.2. Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya

3.Ujenzi huu pia ulianza mwaka 2017 na kwa sasa mradi upo katika hatua ya umaliziaji. Jumla ya Shilingi 650,101,425.67 zimekisiwa kutumika mpaka kukamilika kwa mradi. Mradi umefikia hatua ya umaliziaji.



***Picha* 17: Jengo la Ofisi ya mkuu wa Wilayalinaloendelea kujengwa eneo la Makao Makuu Rubwera**

### 2.6.3. Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya

Ujenzi wa hospitali ya Wilaya ulianza mwaka 2019 baada ya Halmashauri kupata fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Jumla ya Shilingi 1,800,000,000 zimetumika kukamilisha majengo 7 ya hospitali na imeanza kutoa huduma kwa Wananchi.



*Picha 18: Moja ya jengo katika majengo ya Hospitali ya Wilaya yaliyojengwa*

### 2.6.4. Ujenzi wa nyumba ya kuishi ya Mkuu wa Wilaya na Katibu Tawala Wilaya

Nyumba hizi zimejengwa eneo la Kagenyi mlimani karibu na Hospitali ya Wilaya. Nyumba ya Katibu Tawala imekamilika na inatumika na nyumba ya Mkuu wa Wilaya ipo hatua ya umaliziaji. Ujenzi wa nyumba zote mpaka kukamilika umekisiwa kutumia jumla ya Shilingi 657,826,523.03 (Nyumba ya Mkuu wa Wilaya 498,275,525.50 na ya DAS 159,550,997.53). Nyumba ya Katibu Tawala imekamilika na inatumika na nyumba ya Mkuu wa Wilaya ipo hatua ya umaliziaji.

### 2.6.5. Ujenzi wa miundombinu ya miradi ya maji

Kata ya Kyerwa iliyopo Makao Makuu ya Wilaya miradi ya maji ambayo imegharimu Shilingi 680,000,000 imejengwa na Wananchi wanapata huduma ya maji. Miradi hiyo ni pamoja na ule wa Rwenkorongo na Rubwera ambayo yote ni ya visima virefu vinavyotumia nguvu ya umeme kusukuma maji. Upanuzi wa miradi bado unaendelea katika maeneo jirani ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma ya maji.



*Picha 19: Kibanda cha kuuzia maji Rwenkorongo-Kyerwa*

### 2.6.6. Mradi wa ujenzi wa nyumba za Watumishi eneo la mji wa Rubwera

Mradi huu ulianza mwaka 2014 kwa kuanza na nyumba 6 za Wakuu wa Idara kwa gharama ya zaidi ya Shilingi 600,000,000. Nyumba hizo 6 zilikamilika mwaka 2016 na zinatumiwa na Wakuu wa Idara. Aidha nyumba nyingine 2 (2 in1 kila moja) zipo hatua ya umaliziaji kwa fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri.





***Picha 20 Nyumba za Wakuu wa Idara (Juu, zinatumika) na za Watumishi wa kawaida zinazoendelea kujengwa (Chini)***

### 2.6.7. Ujenzi wa kipande cha barabara KM.1 kiwango cha lami katika barabara za mji wa Rubwera

Mradi huu ulijengwa na kuwekewa jiwe la Msingi na Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru za mwaka 2018. Kipande hiki cha lami kiligharimu Shilingi 200,000,000 mpaka kukamilika na kinatumika.

### 2.6.8. Ujenzi wa Maabara za Sayansi na vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Kyerwa

Serikali imejenga maabara hizo kwa gharama ya Shilingi 90,000,000 ikiwa ni fedha za mchango wa Halmashauri na nguvu za Wananchi ili kuhakikisha mazingira ya kujifunzia wanafunzi yanaboreshwa. Aidha katika kuongeza miundombinu shuleni hapo vyumba 4 vya madarasa vimejengwa kwa gharama ya Shilingi 76,000,000 kwa fedha za mchango wa halmashauri na nguvu za Wananchi na vinatumiwa na Wanafunzi.

### 2.6.9. Mradi wa Kitalu nyumba cha Kikundi cha Vijana Kyerwa

Mradi huu unaendeshwa na Kikundi cha Vijana wanaojihusisha na kilimo cha mbogamboga na matunda katika mji wa Rubwera. Mradi huu ulifadhiliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na kuchangiwa fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri na kufanya jumla ya Shilingi 9,550,000 kutumika na unaendelea kunufaisha jamii kupitia kikundi hicho cha vijana.



*Picha 21: Kitalu nyumba cha Kikundi cha Vijana Kyerwa*

**2.6.10. Ukamilishaji wa chumba cha darasa Shule ya Msingi Kagenyi**

Ujenzi wa chumba kimoja cha darasa, Maktaba na Matundu 20 ya vyoo Shule ya Msingi Kagenyi ambao uligharimu kiasi cha Shilingi 39,623,429.25.

Mradi huu ulitekelezwa kuanzia mwaka 2019 hadi 2020 kwa fedha za Mfuko wa jimbo, Nguvu za wananchi, fedha za P4R pamoja na fedha za ufadhili wa Banki ya dunia kupitia Programu ya Usambazaji maji vijijini (SRWSS) Aidha, mradi wa chumba cha darasa na maktaba uligharimu Shilingi 16,314,500. Kutoka Mfuko wa jimbo, P4R na nguvu za wananchi. Vilevile mradi wa matundu ya vyoo ambao hadi sasa uko hatua ya ukamilishaji, umegharimu kiasi cha Shilingi 23,298,929.25, fedha hizi zinatokana na ufadhili wa Benki ya dunia kupia Programu ya Usambazaji maji vijijini (SRWSS) pamoja na nguvu za wananchi



***Picha 22: Chumba cha darasa kilichokamilika na kinatumika Shule ya Msingi Kagenyi***



*Picha 23: Ujenzi wa Matundu ya vyoo Shule ya Msingi Kagenyi na yanatumika*

#### 2.6.11. Ukarabati wa zahanati ya Kagenyi

Mradi wa ukarabati wa zahanati ya kagenyi kwa kufanya marekebisho ya jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la kliniki pamoja na jengo la kina mama. Ukarabati huu uliofanyika na kukamilika mwaka 2018 kwa gharama ya Shilingi 3,000,000 kutoka mfuko wa RBF.



*Picha 24: Jengo la Wagonjwa wa nje lililokarabatiwa katika Zahanati ya Kagenyi*

### 2.7. KATA RUKURAIJO

Kata ya Rukuraijo imetekeleza miradi 13 yenye thamani ya Shilingi **607,445,948.81** Miradi hiyo imetekelezwa katika sekta za Elimu, Afya, Maji, Kilimo na Mifugo**.** Miradi hii ambayo ipo katika hatua mbalimbali, imetekelezwa kupitia fedha toka Serikali Kuu, mfuko wa jimbo, Halmashauri ya Wilaya, Wadau wa Maendeleo na nguvu za

wananchi. Mchanganuo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kata rukuraijo ni kama ifustavyo:-

**2.7.1. Ujenzi wa vyumba vya madarasa, ukarabati wa madarasa 4 na ujenzi wa vyoo**

***matundu 10 Shule ya Sekondari Rukuraijo***

Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa, na ujenzi wa matundu 8 ya vyoo Rukuraijo Sekondari kwa Shilingi 70,000,000.00, na mradi ulitekelezwa mwaka 2016 umekamilika kwa fedha za Serikali Kuu.

**2.7.2. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa, stoo na jiko, ukarabati wa vyumba 6 vya madarasa pamoja na utengenezaji wa madawati 100 Shule ya Msingi Rukuraijo**

Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa, stoo na jiko, ukarabati wa vyumba 6 vya madarasa pamoja na utengenezaji wa madawati 100 Shule ya Msingi Rukuraijo kwa Shilingi 78,840,000. Miradi hii ilitekelezwa mwaka 2019 chuni ya ufadhili wa Banki ya CRDB Miradi imekamilika na inatumika.

**2.7.3. Ujenzi wa vyoo Shule ya Msingi Rukuraijo**

Ujenzi wa matundu 13 ya vyoo Shule ya Msingi. Rukuraijo13kwa gharama ya Shilingi 8,00,000.00 kutoka Mfuko wa Jimbo na nguvu za Wananchi. Mradi ulitekelezwa mwaka 2018, umekamilika na unatumika.



*Picha 27: Ujenzi wa madarasa na ukarabati Shule ya Msingi Rukuraijo*

**2.7.4. Ujenzi wa vyoo Shule ya Msingi Rukuraijo**

Ujenzi wa matundu 8 ya vyoo Shule za Msingi Nyabikurungo kwa ujumla Shilingi 6,000,000.00 kwa fedha za P4R na nguvu za Wananchi. Mradi ulitekelezwa mwaka 2016 umekamilika na unatumika.

**2.7.5. Ujenzi wa madarasa na vyoo Shule ya Msingi Mkombozi**

Ujenzi wa Chumba 1 cha darasa na matundu 6 ya vyoo Shule za Msingi mkombozi kwa ujumla Shilingi 20,000,000.00 kwa fedha za P4R na nguvu za Wananchi. Mradi ulitekelezwa mwaka 2016, umekamilika na unatumika.

**2.7.6 Ukamilishaji wa nyumba ya mwalimu Shule ya Msingi Mkombozi**

Ukamilishaji wa nyumba moja ya walimu (2in1) Shule ya Msingi Mkombozi kwa fedha za P4R na nguvu ya Wananchi. Mradi ulitekelezwa mwaka 2017, nyumba imekamilika na inatumika.

***2.7.7.* Ujenzi wa vyumba vya Maabara Shule ya Sekondari Rukuraijo**

Ujenzi wa vyumba 3 vya maabara Shule ya Sekondari Rukuraijo kwa Shilingi 69,000,450 kutoka Halmashauri (67,500,450) na nguvu ya jamii (15,000,000). Madi ulitekelezwa mwaka 2017, maabara zimekamilika na zinatumika.



***Picha 25: Vyumba vya madarasa Rukuraijo Shule ya Sekondari***

***2.7.8. Ujenzi wa madarasa na vyoo pamoja na ununuzi wa mashine ya urudufishaji (Photocopy machine) Shule ya Sekondari Rukuraijo***

Ujenzi wa vyumba 03 vya madarasa na matundu 10 ya vyoo shule ya sekondari Rukuraijo.Vyumba vya madarasa vilijengwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia, Fedha za Halmashauri na nguvu za wananchi kwa Shilingi Shilingi 72,003,075.00 mwaka 2017, madarasa yamekamilika na yanatumika. Pia umetekelezwa mradi wa ujenzi wa matundu 10 ya vyoo Shule ya Sekondari Rukuraijo kwa gharama ya Shilingi 20,000,000 kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Matundu ya vyoo yamekamilika na yanatumika. Vilevile, Ununuzi wa mashine za kurudufu (Photocopier) ambao umegharimu Shilingi 2,500,000 kutoka Mfuko wa Jimbo ,mashine imenunuliwa na inatumika.

### 2.7.9. Ukarabati wa mradi wa Maji Rukuraijo na Kagenyi

Ukarabati na upanuzi wa mradi wa maji Rukuraijo na Kagenyi uligharimu Shilingi 128,581,048.81 kutoka Serikali Kuu. Hivyo, ukarabati wa miundombinu ya maji ulifanyika na kukamilika na unahudumia Wananchi.

### 2.7.10. Ujenzi wa tanki la maji na miundombinu ya taka katika zahanati ya Rukuraijo

Ujenzi wa tanki la maji zahanati ya Rukuraijo, kizimba cha kuchoma taka na shimo la kutupa kondo la nyuma kwa Shilingi 7,975,500 kutoka Halmashauri mwaka 2018, ujenzi umekamilika na unakamilika.



***Picha 26: Tanki la maji Zahanati ya Rukuraijo***

### 2.7.11. Ukarabati wa barabara za mitaa na makalvati katika kata ya Rukuraijo

Serikali imekarabati barabara km 33,1 na kalvati 6 kwa Shilingi 72,848,000 fedha za Serikali kupitia TARURA, Hivyo, miundombinu ya barabara imeboreshwa na kutumiwa na wananchi.

### 2.7.12. Upandaji miti katika kata ya Rukuraijo

Serikali imepandwa jumla ya miti 83,160 ya aina mbalimbali kwa gharama ya Shilingi 39,000,000 katika vijiji vyote vya Kata ya Rukuraijo fedha zilizotolewa na Halmashauri ya Wilaya.

### *2.7.13. Kuwezesha vikundi vya Wajasiriamali*

Uwezeshaji wa vikundi vya ujasiliamali kwa kutoa mkopo wa Shilingi 5,000,000 kwenye Kikundi kimoja cha wanawake cha UPEO kilichopo Kijiji cha Rukuraijo, fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kiuchumi mwaka 2019.

### 2.7.14. Uwekezaji katika uvuvi wa samaki

Serikali imewezesha upandikizaji wa vifaranga vya samaki 35,000 katika Ziwa Rushwa kwa gharama ya Shilingi 8,500,000. Mradi umekamilika na shughuli za

uvuvi katika ziwa hili zimezuiwa mpaka Septemba 20, 2020 kwa lengo la mavuno ya samaki ya uhakika.

### 2.7.15. Ujenzi wa Ofisi ya Kata Rukuraijo

Serikali imewezesha umaliziaji wa Ofisi ya Kata Rukuraijo mwaka 2018 kiasi cha Shilingi 21,697,875. Ikiwa, Shilingi 19,197,875 ni fedha za Halmashauri na michango ya Jamii ni Sh 2,500,000, mradi umefikia hatua za ukamilishaji.

## 2.8. KATA ISINGIRO

Serikali imetekeleza miradi 15 yenye thamani ya Shilingi **292,955,306.60** katika Kata ya Isingiro. Miradi imetekelezwa sekta za Elimu, Afya, Maji na Umeme. Miradi hii ambayo ipo katika hatua mbalimbali imetekelezwa kupitia fedha za Serikali Kuu, Mfuko wa Jimbo, Halmashauri, Wadau wa maendeleo na nguvu za Wananchi. Mchanganuo wa utekelezaji wa miradi Kata ya Isingiro ni kama ifuatavyo:-

### *2.8.1.* Ujenzi wa matundu 22 ya vyoo Shule ya Msingi Kihanga

Ujenzi wa matundu 22 ya vyoo S/M Kihanga kwa gharama ya Shilingi 26,278,000.00 ikiwa ni fedha za ufadhili wa Benki ya dunia kupitia wakala wa usambazaji wa maji vijijini na usafi wa mazingira (SRWSS) na nguvu ya Wananchi. Mradi ulianza kutekelezwa mwaka 2020 na uko hatua za umaliziaji.

### 2.8.2. Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Katera

Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Katera. Ambao uligharimu Jumla ya Shilingi 25,278,000, ikiwa ni nguvu za Wananchi. Mradi ulianza mwaka 2017 na umefikia hatua ya linta.



**Picha 32: Jengo la zahanati ya Kijiji cha Katera linaloendelea kujengwa**

**2.8.3. Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Kihanga**

Ujenzi wa zahanati Kijiji Kihanga, kiasi cha Shilingi 3,350,000 zimetumika ikiwa ni nguvu za jamii na mradi umefikia hatua za awali za ujenzi wa msingi na ujenzi unaendelea

**2.8.4. Ujenzi wa Ofisi ya Kijiji Ibare**

Uendelezaji wa ujenzi wa ofisi ya Kijiji Ibare kwa gharama ya Shilingi 1,300,000 kwa nguvu za Wananchi umefanyika, mradi upo hatua ya kuezeka na jitihada za kukamilisha zinaendelea.

***2.8.5.* Ujenzi wa Ofisi ya Kijiji Karukwanzi**

Mradi wa ujenzi ofisi ya Kijiji Karukwanzi 'A' unaendelea, Jumla ya Shilingi 6,520,000.00 imetumika ikiwa ni mchango ya Jamii 2,887,209 na Mfuko wa Jimbo 3,632,791. Mradi upo hatua ya ujenzi wa kuta na unaendelea.

***2.8.6.* Ujenzi wa matundu 14 ya vyoo Shule ya Msingi Isingiro**

Ujenzi wa matundu 14 ya vyoo S/M Isingiro kwa gharama ya Shilingi 17,789,929.20 kutoka Serikali Kuu umefanyika, mradi upo hatua za umaliziaji

***2.8.7. Ujenzi wa chumba 1 cha darasa Shule ya Msingi Ishaka***

Uendelezaji wa ujenzi wa chumba 01 cha darasa S/M Ishaka umefanyika, kiasi cha Shilingi 1,300,000 kutoka mfuko wa Jimbo zimetumika, mradi unaendelea.

**2.8.8. *Ujenzi wa vyumba 2 vya madarsa Shule ya Sekondari Isingiro***

Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa shule ya sekondari ya Isingiro, Kiasi cha Sh 21,000,000 ikiwa ni nguvu ya Jamii na mchango wa Halmashauri imetumika na vyumba vimeezekwa na vipo hatua za umaliziaji.

### 2.8.9. Ujenzi wa chumba 1 cha darasa Shuke ya Msingi Karukwanzi

Ukamilishaji wa chumba 1 cha darasa s/m Karukwanzi umegharimu Shilingi 12,500,000.00, fedha kutoka Serikali Kuu, mradi umekamilika na unatumika

### 2.8.10. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Isingiro

Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Isingiro umefanyika kwa gharama ya Shilingi 38,941,200.00, fedha za ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, AfDB, mradi umekamilika na unatumika



***Picha 27: Vyumba 2 vya madarasa kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo Afrika Shule ya Sekondari Isingiro***

### 2.8.11. Ukamilishaji wa chumba cha darasa na nyumba ya Walimu Shule ya Msingi Ibare

Ukamilishaji wa nyumba ya Walimu na chumba cha darasa S/M Ibare umefanyika kwa jumla ya Shilingi 15,097,133.40 kutoka Serikali Kuu, mradi unatumika.

### 2.8.12. Ukamilishaji wa nyumba ya Mwalimu (2 in 1) Shule ya Msingi Ishaka

Ukamilishaji wa nyumba ya mwalimu 2in1 S/M Ishaka umefanyika, jumla ya Shilingi 1,500,000 kutoka Mfuko wa Jimbo zimetumika na mradi umekamilika

### 2.8.13. Ukarabati wa madarasa, kisima cha maji na vyoo Shule ya Sekondari Isingiro

Ukarabati wa madarasa 5, kisima cha maji na ujenzi wa matundu 10 ya vyoo Isingiro Sekondari umefanyika kwa Shilingi 113,750,000.00 kutoka Serikali Kuu. Madarasa 5 yamekarabatiwa pamoja na kisima cha maji, matundu 10 ya vyoo yamejengwa na kukamilika na yanatumika.

### 2.8.14. Ujenzi wa chumba cha darasa Shule ya Sekondari Isingiro

Ukamilishaji wa chumba 1 kimoja cha darasa ISingiro Sekondari kwa Shilingi 7,351,044.00 kwa fedha kutoka serikalini umefanyika, chumba kimekamilika na kinatumika.

### 2.8.15. Ujenzi wa Cliniki ya mama na motto Kijiji cha Kaitambuzi

Kusaidia Ujenzi wa cliniki ya mama na mtoto Kijiji cha Kaitambuzi kwa Shilingi 1,000,000 kutoka Mfuko wa Jimbo umefanyika, cliniki imekamilika na inahudumia wananchi.

## 2.9. KATA KAISHO

Serikali imetekeleza miradi 15 yenye thamani ya Shilingi **1,036,200,418.03** ndani ya kata kaisho katika shule za Msingi, Sekondari, Sekta ya Maji na Vituo vya kutolea huduma za Afya. Miradi hii ambayo ipo katika hatua mbalimbali imetekelezwa kupitia fedha zilizotolewa na Serikali Kuu, Mfuko wa Jimbo, mchango wa Halmashauri, Wadau wa Maendeleo na nguvu za Wananchi. Mchanganuo wa utekelezaji miradi katika Kata ya Kaisho ni kama ifuatavyo:-

### 2.9.1. *Mradi wa maji Kaisho – Isingiro*

Ukarabati na upanuzi wa mradi wa maji Kaisho-Isingiro umefanyika kwa Shilingi 649,345,900.00 fedha kutoka Serikali Kuu, mradi unaendelea kukarabatiwa na umeanza kutoa huduma kwa Wananchi.

### 2.9.2. *Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Nyabishenge*

Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa, ukarabati wa vyumba 3 vya madarasa Nyabishenge Sekondari kwa Shilingi 128,134,000.00 kutoka Serikali Kuu umefanyika, ujenzi umekamilika na mradi unatumika.



*Picha 28: Vyumba vya madarasa vya P4R Shule ya Sekondari Nyabishenge*

### *2.9.3.* Ujenzi wa bweni la Wasichana Shule ya Sekondari Nyabishenge

Ujenzi wa bweni kwa ajili ya kidato cha tano na sita Nyabishenge Shule ya Sekondari kwa umefanyika kwa ghara ya Shilingi 53,709,400.00, fedha za ufadhili wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), mradi umekamilikana.

**2.9.4. *Ukarabati wa vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Nyabishenge***

Ukarabati wa vyumba 2 vya madarasa na nyumba ya mwalimu Nyabishenge Sekondari Shilingi 14,324,157.00 umefanyika kwa fedha kutoka Serikali Kuu. Ukarabati umefanyika na kukamilika.

**2.9.5. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Nyabishenge**

Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Nyabishenge Sekondari umefanyika kwa gharama ya Shilingi 42,580,300.38, fedha kutoka Serikali Kuu, ujenzi umekamilika na madarasa yanatumika.

**2.9.6. *Ujenzi wa nyumba ya Afisa Tarafa Kaisho***

Ujenzi wa nyumba kwa ajili ya Afisa Tarafa Kaisho umefanyika, mradi huu umegharimu jumla ya Shilingi 52,636,049.40 fedha zilizotolewa na Serikali Kuu. Mradi huu umekamilika.



***Picha 29: Jengo la Ofisi ya Afisa Tarafa Kaisho***

***2.9.7.* Uwezeshaji wa mashine ya fotokopia na ujenzi wa vyumba vya madarasa Nyabishenge Sekondari**

Ununuzi wa photocopier Nyabishenge Shule ya Sekondari kwa fedha za Mfuko wa Jimbo Shilingi 3,000,000.00 umefanyika, mashine imenunuliwa na inatumika. Pia ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa kwa gharama ya Shilingi 3,500,000 fedha kutoka mfuko wa Jimbo na nguvu za Wananchi umeendelea na jengo liko hatua ya uezekaji.

**2.9.8. *Ujenzi wa matundu ya vyoo Shule ya Msingi Kaisho***

Kusaidia ujenzi wa matundu 2 ya vyoo S/M Kaisho kwa Sh 1,000,000 umefanyika kwa fedha toka Mfuko wa Jimbo, vyoo vimejengwa na vinatumika

**2.9.9. Ukamilishaji wa vyumba vya madarasa Shule za Msingi Rwakiniha na Rwamashaju**

Ukamilishaji wa chumba 1 cha darasa S/M Rwakiniha umegharimu Shilingi 1,500,000 nguvu za jamii. Chumba kimoja 1 cha darasa kimekamilika na kinatumika na pia chumba 1 cha darasa S/M Rwamashaju kimekamilika na kinatumika ikiwa ni fedha kutoka Mfuko wa Jimbo.

***2.9.10. Ujenzi wa vyoo Shule ya Msingi Nyabishenge***

Ujenzi wa matundu 4 ya vyoo s/m Nyabishenge umefanyika kwa kwa ufadhili wa Chama cha msingi Kaisho kwa gharama ya Shilingi 500,000.00 na nguvu za Wananchi, mradi umekamilika na unatumika.

**2.9.11. Ujenzi wa Maabara na stoo zahanati ya Kaisho**

Ujenzi wa vyumba 2 vya maabara na stoo ya madawa zahanati ya Kaisho umefanyika kwa gharama ya Shilingi 9,354,000, fedha za RBF, mradi upo hatua ya umaliziaji.

**2.9.12. Ujenzi wa matundu 20 ya vyoo Shule ya Msingi Kaisho**

Matundu 20 ya vyoo S/M Kaisho kwa umekamilika kwa gharama ya Shilingi 19,467,929.25 kwa ufadhili wa Benki ya dunia kupitia Wakala wa Programu ya usambazaji maji vijijini na usafi wa mazingira (SRWSS). Ujenzi umekamilika.

**2.9.13. Ujenzi wa Ofisi ya Kata Kaisho**

Ujenzi wa ofisi ya Kata Kaisho umefanyika kwa gharama ya Shilingi 48,148,682, fedha za Mfuko wa Jimbo, mchango wa Halmashauri na nguvu za jamii, ujenzi umekamilika na ofisi inatumia.



***Picha 30: Jengo la Ofisi ya Kata ya Kaisho***

***2.9.14. Ujenzi wa Ofisi ya Kijiji Chababara***

Serikali imesaidia ujenzi wa Ofisi ya Kijiji Chababara kwa gharama ya Shilingi 2,000,000, fedha kutoka Mfuko wa Jimbo, mradi upo hatua ya umaliziaji.

***2.9.15. Uboreshaji wa barabara Kaisho – Chababara na Nyabishenge - Rwakiniha***

Uboreshaji wa km 7 za barabara ya kutokea Kaisho – Chababara na Nyabishenge – Rwakiniha umefanyika kwa gharama ya Shilingi 7,000,000 kupitia Mfuko wa Barabara, barabara inatumika.

## 2.10. KATA NYARUZUMBURA

Serikali katika Kata ya Nyarunzumbura imetekeleza miradi 5 yenye thamani ya Shilingi **100,600,000.00** katika sekta za Elimu, na Afya. Miradi hii ambayo ipo katika hatua mbalimbali, imetekelezwa kupitia fedha Serikali Kuu, Mfuko wa Jimbo, mchango wa Halmashauri, Wadau wa Maendeleo na nguvu za Wananchi. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-



***Picha 31: Ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Nyaruzumbura***

**2.10.1.** ***Ujenzi wa vyoo Shule ya Msingi Nyaruzumbura***

Kukamilisha ujenzi wa matundu 4 ya vyoo S/M Nyaruzumbura umefanyika kwa gharama ya Shilingi 2,000,000 kutoka Mfuko wa Jimbo, mradi umekamilika na unatumika.

**2.10.2.** ***Ukamilishaji wa vyumba 3 vya madarasa na Ofisi Shule ya Msingi Omukiyonza***

Kusaidia uezekaji wa vyumba 3 vya madarasa na Ofisi S/M Omukiyonza, Mfuko wa Jimbo Shilingi 2,000,000, mchango wa halmashauri 3,375,000 na nguvu ya Jamii 1,600,000 Ujenzi upo katika hatua ya umaliziaji.

**2.10.3.** ***Ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Nyaruzumbura***

Ukamilishaji wa vyumba 5 vya madarasa Shule ya Sekondari Nyaruzumbura umeendelea kwa gharama ya Shilingi 60,000,000 ikiwa ni wa nguvu ya Jamii na mchango wa Halmashauri, mradi uko hatua za umaliziaji.

**2.10.4.** ***Ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Msingi Nyaruzumbura***

Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa S/M Nyaruzumbura kwa gharama ya Shilingi 18,600,000 umefanyika kwa fedha za Halmashauri na nguvu ya Jamii, mradi uko hatua za umaliziaji.

**2.10.5** ***Ujenzi wa zahanati ya Kijiji Milambi***

Ujenzi wa zahanati ya Milambi umeendelea kwa gharama ya Shilingi 18,000,000 ikiwa ni nguvu za Wananchi, mradi upo hatua za awali za ujenzi wa msingi, mradi unaendelea.

## 2.11. KATA KIKUKURU.

Kata Kikukuru imetekeleza miradi yenye thamani ya Shilingi **168,880,300.00** katika shule za Msingi za Rubilizi, Kikukuru, Karambi, Rwele, Sekondari ya Mukire na Vituo vya kutolea huduma za Afya vya Rwele, Karambi, na Kikukuru, kutokana na Fedha za Nguvu za Wananchi, ADB,P4R, RBF na Mfuko wa Jimbo**.** Miradi hii inafafanuliwa kwa kina katika aya zinazofuata.

### *2.11.1* Ujenzi wa zahanati ya Kijiji Omukitembe

Uendelezaji wa ujenzi wa Zahanati ya Mukunyu na Omukatembe ambao umegharimu kiasi cha Shilingi 23,500,000.00, fedha zilizotokana na Nguvu za Wananchi umefanyika. Mradi huu ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2011, hadi sasa mradi umefikia hatua ya umaliziaji na ujenzi unaendelea.

### 2.11.2 Ujenzi wa bweni la Wavulana Shule ya Sekondari Mukire

Ujenzi wa Bweni la Wavulana Shule ya Sekondari Mukire ambao umegharimu Shilingi 26,021,000.00 kutokana na Nguvu za wananchi. Mradi ulianza kutekelezwa mwaka 2020, ujenzi unaendelea kukamilishwa na unatumiwa na wanafunzi wapatao 120.

### 2.11.3. Ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Mukire

Ujenzi wa Vyumba 2 vya madarasa Mukire Sekondari umegharimu Shilingi 39,019,200.00 kutokana na fedha za ufadhili wa Benki ya Maendeleo Afrika, ADB. Mradi ulianza mwaka 2017, umekamilika na unahudumia wanafunzi 90.

### *2.11.4. Ukarabati na ujenzi wa mashimo ya kuchoma taka na kondo la nyuma zahanati ya Rwele*

I. Ujenzi wa shimo la kutupia kondo la nyuma na ukarabati wa shimo la kuchomea taka katika kituo cha kutolea huduma za Afya Rwele umekamilika. Miradi imegharimu kiasi cha Shilingi 4,986,900.00 kutokana na fedha za RBF, imekamilika na inatoa huduma kwa wananchi wapatao 4,000.

### 2.11.5. *Ukamilishaji wa vyumba vya madarasa na vyoo Shule ya Msingi Karambi*

Ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa na matundu 6 ya vyoo S/M Karambi. Mradi umegharimu kiasi cha Shilingi 16,650,00.00 kutokana na Nguvu za Wananchi. Mradi ulianza mnamo mwaka 2015 ambapo, vyumba 2 vya madarasa vimekamilika na matundu 6 ya vyoo yako hatua ya umaliziaji. Mradi unataraijiwa kuhudumia wanafunzi 125.

**2.11.6.** ***Ujenzi wa zahanati ya Kijiji Karambi***

Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Karambi umegharimu jumla ya Shilingi 2,942,000.00 kutokana na Nguvu za Wananchi. Ulianza mwaka 2016. Mradi unaendelea kutekelezwa.

***2.11.7. Ujenzi wa madarasa, kisima cha maji, vyoo na mfumo wa umeme Shule ya Msingi Rubilizi***

Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa, kisima cha maji, matundu 4 ya vyoo na kuweka mfumo wa umeme Shule ya Msingi Rubilizi umeendelea. Mradi umegahrimu Shilingi 12,300,00.00 kutokana na Nguvu za Wananchi ambapo, matundu 4 ya vyoo na kisima cha maji vimekamilika, vyumba vya madarasa viko hatua ya umaliziaji. Miradi hii inategemewa kuhudumia Wanafunzi wapatao 641.

**2.11.8.** ***Ujenzi wa matundu ya vyoo na bafu zahanati ya Kikukuru***

Ujenzi wa matundu 2 na mabafu 2 Zahanati ya Kikukuru umegharimu Shilingi 6,800,000.00 kutokana na fedha za RBF. Mradi ulianza mwaka 2018, umekamilika na unahudumia wananchi.

**2.11.9. Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje, OPD Zahanati ya Kijiji cha Rwele**

Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) katika zahanati ya Rwele umegharimu kiasi cha Shilingi 133,345,330 Ikiwa Shilingi 125,345,330.00 ni kutoka Mfuko wa Maafa Mkoa wa Kagera na 8,000,000 mchango wa Halmashauri katika ujenzi huo. Jengo limekamilika na linatumika kutoa huduma kwa Wananchi.

**2.11.10. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Msingi Kikukuru**

Mradi wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika Shule ya Msingi Kikukuru umefadhiliwa na Shirika la Maendeleo Duniani (UNDP) kwa kushirikiana na Serikali ya Afrika Kusini ikiwa ni katika kusaidia kurejesha miundombinu iliyoathiriwa na Tetemeko la Ardhi lililotokea Septemba 10, 2016. Mradi huu umegharimu jumla ya Shilingi 48,961,200 na umekamilika.



*Picha 32: Vyumba vya madarasa Shule ya Msingi Kikukuru*

## 2.12. KATA YA NYAKATUNTU

Serikali katika Kata ya Nyakatuntu imetekeleza miradi yenye thamani ya Shilingi **98,888,298.00** katika shule za Msingi za Rubilizi, Kikukuru, Karambi, Rwele, Sekondari ya Mukire na Vituo vya kutolea huduma za Afya vya Rwele, Karambi, na Kikukuru ambayo iko katika hatua mbalimbali. Miradi hii imetekelezwa kwa Fedha za Nguvu za wanchi, Fedha za Serikali na Mfuko wa Jimbo. Ufafanuzi wa kina juu ya miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

### 2.12.1. Ujenzi wa madarasa Shule ya Msingi Nyakatuntu

Mradi wa ujenzi wa Vyumba 3 vya Madarasa Nyakatuntu s/m umegharimu kiasi cha Shilingi 48,961,200.00 fedha kutoka ufadhili wa Shirika la Maendeleo Duniani, UNDP ikiwa ni juhudi za kurejesha miundombinu iliyoathiriwa na Tetemeko la Ardhi. Mradi ulianza utekelezaji mwishoni mwa mwaka 2019 na umekamilika.



*Picha 33: Vyumba vya madarasa Shule ya Msingi Nyakatuntu*

**2.12.2.** ***Ujenzi wa matundu ya vyoo Shule ya Msingi kasoni***

Mradi wa ujenzi wa matundu mawili ya vyoo S/M kasoni umegharimu Shilingi 3,918,000.00 kutokana na mchango wa Halmashauri na Nguvu za Wananchi. Mradi ulianza kutekelezwa mwaka 2019 na ujenzi unaendelea.

**2.12.3.** ***Kukamilisha ujenzi wa madarasa na Ofisi ya Mwalimu Shule ya Msingi Rukili***

Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na Ofisi ya Walimu S/Msingi Rukiri umegharimu kiasi cha Shilingi 13,562,500.00 kutokana na Nguvu za Wananchi. Mradi umefikia hatua ya ukamilishaji na unatarajiwa kuhudumia wanafunzi wapatao 90.

**2.12.4.** ***Ujenzi wa zahanati ya Kijiji Nyakatuntu***

Jengo la wagonjwa wa nje, 'OPD' na jengo la huduma za mama na mtoto, 'RCH' zahanati ya Nyakatuntu umegharimu kiasi cha Shilingi 8,658,557.00 kutokana na Fedha za ufadhili wa Chama cha Msingi Nyakatuntu na Chama cha Msingi Kasoni. Mradi unaendele kutekelezwa.

**2.12.5.** ***Ujenzi wa madarasa na vyoo Shule ya Sekondari Nakake***

Ujenzi wa vyumba viwili vya Madarasa matundu mawili ya Choo S/Sekondari Nakake umegharimu kiasi cha Shilingi 23,788,041.00 kutokana na fedha kutoka Serikali Kuu na Nguvu za Wananchi. Vyumba vimekamilika na vinatumika.

## 2.13. KATA YA KAKANJA

Serikali katika Kata ya kakanja kwa kipindi cha miaka 5 kuanzia mwaka 2015-2020 imetekeleza miradi mbalimbali yenye thamani ya Shilingi **130,264,270.25** kama ifuatavyo:-

**2.13.1.** ***Ujenzi wa vyoo Shule ya Msingi Kakanja***

Ujenzi wa matundu 37 ya vyoo S/M Kakanja umegharimu kiasi cha Shilingi 46,674,929.25, fedha za ufadhili wa Benki ya dunia kupitia wakala wa Usambazaji Maji vijijini na Usafi wa mazingira (SRWSS) pamoja na Nguvu za Wananchi. Mradi ulianza mwaka 2016 kwa matundu ya vyoo 4 ambayo yamekamilika na yanatumika. Aidha, ujenzi wa matundu mengine 33 ya vyoo unaendelea na uko hatua ya umaliziaji.



*Picha 34: Ujenzi wa matundu ya vyoo Shule ya Msingi Kakanja*

**2.13.*2. Ujenzi wa madarasa na ukarabati Shule ya Msingi kakanja***

Ujenzi wa vyumba 2 na ukarabati wa chumba 1 cha darasa S/M Kakanja umegharimu jumla ya Shilingi 28,000,000 kutokana na Nguvu za Wananchi pamoja na Fedha kutoka Serikali Kuu. Mradi ulianza mwaka 2012 na kukamilika 2020 ambapo unahudumia wanafunzi wapatao 135.



*Picha 35: Vyumba 2 vya madarasa na ukarabati Shule ya Msingi Kakanja*

**2.13.3. *Ujenzi wa nyumba ya Mwalimu Shule ya Msingi kakanja***

Ujenzi wa Nyumba ya Walimu S/Msingi Kakanja umegharimu jumla ya Shilingi 31,801,300 kutokana na michango ya Wananchi, Mkuu wa Wilaya pamoja na Fedha kutoka Serikali Kuu. Mradi ulianza mwaka 2016 na umefikia hatua ya umaliziaji.

**2.13.3. *Ujenzi wa nyumba ya kupumzikia wagonjwa na shimo la kutupa kondo la nyuma***

IV Ujenzi wa nyumba ya kupumzika wagonjwa pamoja na ukarabati wa shimo la kutupa kondo la nyuma pamoja na ujenzi wa matundu manne ya vyoo katika kituo cha kutolea huduma za Afya Kakanja umegharimu kiasi cha Shilingi 23,788,041.00 kutokana na Fedha za RBF, Mfuko wa Jimbo na Nguvu za Wananchi. Miradi ilianza kutekelezwa mwaka 2017 na kukamilika mwaka 2018 ambapo wananchi wapatao 11,830 wananufanufaika na miradi hiyo.

## 2.14. KATA YA KIMULI

Kata kimuli imetekeleza miradi yenye thamani ya Shilingi **148,546,776.00** katika sekta za Elimu Msingi, Sekondari na Vituo vya kutolea huduma za Afya. Miradi hiyo imefikia hatua mbalimbali kama inavyofafanuliwa hapa chini:-

### 2.14.1. *Ujenzi wa chumba cha darasa na matundu ya vyoo Shule ya Sekondari Kimuli*

Ujenzi wa chumba cha darasa na matundu 8 ya vyoo S/Sekondari Kimuli umegharimu kiasi cha Shilingi 17,000,00.00 kutokana na mchango wa Halmashauri pamoja na Michango ya Nguvu za Wananchi. Mradi ulianza mnamo mwaka 2019, kufikia sasa chumba cha darasa kimefikia hatua ya uezekaji na matundu ya vyoo yamefikia hatua ya umaliziaji. Miradi inatarajiwa kuhudumia wanafunzi wapatao 439.

### 2.14.2. *Ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo Shule ya Msingi Kimuli*

Ujenzi na ukamilishaji wa vyumba 4 vya madarasa na matundu ya vyoo S/Msingi Kimuli umegharimu kiasi cha Shilingi 49,620,000.00 kutokana na mchango wa Halmashauri na Nguvu za Wananchi. Aidha, vyumba viwili vilivyojengwa vimefikia hatua ya usawa wa linta,na vyumba viwili vimeezekwa. Miradi hii inatarajia kuhudumia wanafunzi wapatao 1,574 pindi itakapo kamilika.



***Picha 36: Ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Msingi Kimuli***

### 2.14.3. *Ujenzi wa zahanati ya Kijiji Rwanyango*

Mradi wa ujenzi wa kituo cha kutolea huduma za Afya katika Kijiji cha Rwanyango ambao unakadiriwa kukamilika kwa gharama ya Shilingi 190,000,000.00 kwa fedha kutoka Serikali Kuu, mchango wa Halmashauri na Nguvu za Wananchi. Ujenzi ulianza mwaka 2010 mpaka sasa umefikia hatua ya Linta. Mradi unatarajiwa kuhudumia wananchi Wapatao 12,645 pindi utakapokamilika.

### 2.14.4. *Ujenzi wa jengo la utawala Rwanyango Shule ya Msingi*

Ujenzi wa jengo la Utawala S/Msingi Rwanyango umegharimu kiasi cha Shilingi 30,000,000.00, fedha kutokana na mchango wa Halmashauri na Nguvu za Wananchi. Mradi uko hatua ya Msingi na ulianza mwaka 2018 na ujenzi unaendelea.

**2.14.5. *Ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo Shule ya Msingi Rwanyango***

Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na matundu 8 ya vyoo S/M Rwanyango umegharimu jumla ya Shilingi 61,432,566.00, fedha za ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ikiwa ni juhudi za urejeshaji wa miundombinu iliyoathiriwa na Tetemeko la Ardhi Septemba 10, 2016.

**2.14.6. *Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi Shule shikizi ya Chakalisa***

Ujenzi wa vyumba 2 vya darasa na Ofisi ya Walimu kwa ajili ya Shule shikizi Chakalisa umegharimu Shilingi 37,494,210 kutokana na Mchango wa Halmashauri na Nguvu za Wananchi. Ujenzi ulianza mwaka 2018 na mpaka sasa limefikia usawa wa Linta na ujenzi unaendelea.

## 2.15. KATA YA RWABWERE

Kata ya Rwabwere imetekeleza miradi ya maendeleo mbalimbali katika sekta za elimu, afya na utawala yenye jumla ya thamani ya Shilingi **108,204,300.00**. Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali, imetekelezwa kupitia fedha serikali Kuu, Mfuko wa Jimbo na nguvu za Wananchi. Mchanganuo wa miradi ni kama ifuatavyo:-

**2.15.1. Mradi wa ujenzi Ofisi ya Kijiji Rwabwere**

Mradi umegharimu Kiasi cha shilingi 12,000,000.Ujenzi ulianza mwaka 2012 na jengo limefikia hatua ya kueezekwa na kupigwa plasta likiwa limekwishaghalimu kiasi cha shilingi 6,800,000 ambazo ni fedha zitokanazo na nguvu za wananchi. Utekelezaji wa mradi unaendelea

**2.15.2. Mradi wa ofisi ya walimu Shule ya Msingi Rwabwere**

Mradi una thamani ya shilingi 9,811,800 ambazo ni Nguvu za wananchi. Mradi umefikia hatua ya kuezekwa na utekelezaji wake bado unaendelea.

***2.15.3. Mradi wa ujenzi wa nyumba ya mganga (Two in One) zahanati ya Karongo***

Mradi una thamani ya shilingi 27,294,500 na umefikia hatua ya kuezekwa.Gharama zilizotumika mpaka sasa ni shilingi 8,366,650 ambazo zimetokana fedha za Serikali Kuu na nguvu za wananchi.Ikiwa jengo bado

halijakamilika, kunahitajika kiasi cha shilingi 18,927,850 ambazo ni gharama za kupiga plasta,kuweka milango, madirisha na kupaka rangi.

### *2.15.4. Mradi wa ujenzi wa nyumba ya mwalimu (Two in One) shule ya msingi Karongo*

Mradi una thamani ya shilingi 27,833,000 na upo hatua ya umaliziaji. Gharama zilizotumika mpaka sasa ni shilingi 27,333,000 ambazo zimetokana fedha za serikali kuu, P4R (25,000,000/=) na nguvu za wananchi (2,333,000/=). Mradi haujakamilika na utekelezaji wake unaendelea.

### 2.15.5. Mradi wa ujenzi wa matundu 8 ya vyoo Shule ya Msingi Nyamweza

Mradi huu una thamani ya shilingi 8,00,000 umeanza mnamo mwaka 2019 kutokana na nguvu za wananchi. Mradi umefikia hatua ya Linta na utekelezaji wake unaendelea.

### 2.15.6. Mradi wa ujenzi ofisi ya kijiji cha Nyamweza

Mradi huu una thamani ya shilingi 12,000,000.na umefikia hatua ya kuezekwa kwa gharama ya Shilingi 5,275,000 ikiwa ni fedha za mfuko wa jimbo (2,000,000) na nguvu za wananchi (3,275,000).Utekelezaji wa mradi unaendelea



***Picha 37: Ujenzi wa Ofisi ya Kijiji cha Nyamweza***

### *2.15.7. Mradi wa ujenzi ofisi ya Kata Rwabwere*

Mradi una thamani ya shilingi 11,265,000 umeanza mnamo mwaka 2008 na umefikia hatua ya kuezekwa ukiwa umegharimu kiasi cha shilingi 5,000,000 00. Fedha za mfuko wa jimbo ni Shilingi 2,000,000/= na nguvu za wananchi ni Shilingi 3,000,000/=. Ukamilishaji wa ujenzi unaendelea.

## 2.16. KATA YA SONGAMBELE

Kata ya Songambele imetekeleza miradi ya maendeleo mbalimbali katika sekta za elimu na afya, yenye jumla ya thamani ya shilingi **618,993,128.50**. Miradi hii ambayo ipo katika hatua mbalimbali, imetekelezwa kupitia fedha za serikali kuu, Mfuko wa Jimbo, Wahisani na nguvu za Wananchi. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

### *2.16.1.* Mradi wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa shule ya sekondari Chanyangabwa

Mradi huu wenye thamani ya shilingi 26,275,850.00 umeanza mnamo mwaka 2018 na chumba kimoja kimeezekwa, wakati chumba kingine kimefikia hatua ya anamu. Gharama zilizotumika mpaka sasa ni shilingi 26,275,850.00 ambazo fedha kutoka Halmashauri (18,999,680.00/=) na nguvu za wananchi (7,276,170.00/=). Chumba kimoja kinahitaji kuezekwa na kufanyiwa umaliziaji. Mradi utakapo kamilika unatarajiwa kuwanufaisha wanafunzi 90 wa shule hii.

### 2.16.2. Mradi wa ujenzi wa matundu 8 ya vyoo shule ya sekondari Songambele

Mradi huu wenye thamani ya shilingi 14,410,000.00 umeanza mnamo mwaka 2019 na upo hatua ya umaliziaji. Jumla ya shilingi 7,774,000.00 ni kutoka Halmashauri, na 6,636,000.00 nguvu za wananchi. Utekelezaji wa mradi unaendelea.

### 2.16.3. Mradi wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Chanyangabwa

Mradi huu una thamani ya shilingi 24,380,000.00 ulianza mnamo mwaka 2019 kutokana na fedha za Halmashauri, Mfuko wa Jimbo na Nguvu za wananchi Utekelezaji wa Mradi unaendelea.

### 2.16.4. Mradi wa ujenzi wa nyumba 1 ya mwalimu Shule ya Sekondari Chanyangabwa

Mradi una thamani ya Shilingi 11,131,250 .kutokana na Fedha za mfuko wa jimbo, nguvu za wananchi. Mradi ulianza mwaka 2019 na umefikia hatua ya linta, Utekelezaji wa Mradi unaendelea.

### 2.16.5. Mradi wa ujenzi wa matundu 4 ya vyoo shule ya msingi Songambele

Ujenzi wa mradi huu ulianza mwaka 2016 na kukamilika mwaka 2017 ukikisiwa kuwa na gharama ya shilingi 4,650,000 na ulidhaminiwa na mfuko wa SWASHILINGI Mradi huu tayari umeishawanufaisha wanafunzi 100.

### 2.16.6. Mradi wa ujenzi wa matundu 20 ya vyoo Shule ya Msingi Songambele

Mradi huu ulitekeleza kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilihusisha matundu 4 ya vyoo ambayo yaligaharimu Shilingi 4,650,000.00 na ulitekelezwa mwaka

2016-2017. Awamu ya pili ya Mradi huu ni ya mwaka 2020 ambayo ilihusisha matundu ya vyoo 16 ambayo yamefikia hatua ya ukamilishaji kwa gharama ya Shilingi 18,464,929.25. Miradi ilitekelezwa kwa fedha kutoka SWASH na utekelezaji wake unaendelea.



**Picha 46: Ujenzi wa matundu 16 ya vyoo shule ya msingi Songambele**

**2.16.7. Mradi wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na ofisi ya waalimu Shule ya Msingi Kitega**

Mradi huu wenye thamani ya shilingi 21,943,215 ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2017, ikiwa kiasi cha shilingi 15,000,000 ni kutoka Serikali kuu,wafadhili shilingi 4,593,215, na kiasi cha shilingi 2,350,000 ni nguvu za wananchi. Mradi umefikia hatua ya umaliziaji na utekelezaji wake unaendelea.

**2.16.8. Mradi wa ujenzi wa matundu 14 ya vyoo vya wanafunzi Shule ya Msingi Chanyangabwa**

Ujenzi wa mradi huu una thamani ya Shilingi 13,500,000.00 ulianza mwaka 2016 kwa ujenzi wa matundu 6 ya vyoo na ulikamilika. Uendelezaji wa mradi wa matundu 8 ya vyoo ulianza mwaka 2020 ambapo shimo limechimbwa na ujenzi unaendelea.

**2.16.9. Mradi wa ujenzi wa chumba cha kujifungulia zahanati ya Songambele**

Mradi huu umeanza kutekelezwa mnamo oktoba, 2018, wenye thamani ya kiasi cha shilingi 30,000,000 ambapo chanzo cha fedha ni kutoka Halmashauri, Wafadhili na nguvu za jamii. Mradi umefikia hatua ya ukamilishaji.



*Picha 47: Nyumba ya kujifungulia akina mama Zahanati ya Songambele*

**2.16.10. Mradi wa ujenzi wa nyumba ya mwalimu Shule ya Msingi Songambele**

Ujenzi wa mradi huu ulianza mnamo mwaka 2016 ukiwa na thamani ya shilingi 5,571,000 .Chanzo cha fedha za mradi huu ni Halmashauri shilingi 3,641,000, na nguvu za jamii shilingi 1,930,000. Hadi sasa jengo lipo katika hatua ya umaliziaji.

**2.16.11. Mradi wa ujenzi wa chumba 1 cha darasa Shule ya Msingi Chanyangabwa**

Ujenzi wa mradi huu ulianza mnamo mwaka 2016 ukiwa na thamani ya jumla ya shilingi 10,500,000. Chanzo cha fedha za mradi huu ni Halmashauri ambayo iliyotoa shilingi 7,000,000 na wanajamii walichangia kiasi cha shilingi 3,500,000. Mradi kwa sasa upo katika hatua ya umaliziaji na utekelezaji wake unaendelea.

**2.16.12. Mradi wa ujenzi wa nyumba 1 ya mwalimu Shule ya Msingi Kasharara**

Ujenzi wa nyumba hii ulianza mnamo mwaka 2015, ukikadiriwa kugharimu jumla ya kiasi cha shilingi 12,516,000.kutokana na fedha za Halmashauri shilingi 7,791,000 na Michango ya jamii kiasi cha shilingi 4,725,000. Mradi upo hatua ya ukamilishaji.

**2.16.13. Mradi wa ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa Shule ya Msingi Kasharara**

Mradi huu ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2018, ukiwa na thamani ya shilingi 60,000,000 na tayari umekamilika mwaka 2019 na unatumika. Mradi huu ulifadhiliwa na Serikali Taasisi ya Elimu, TEA


**Picha 38: Ujenzi wa vyumba vya madarasa shule ya msingi Kasharara**

### 2.16.14. Mradi wa ujenzi wa matundu 6 ya vyoo vya wanafunzi Shule ya Msingi Kasharara

Ujenzi wa matundu haya ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2018 kwa thamani ya Shilingi 6,254,320 kutokana na fedha za Halmashauri pamoja na Nguvu za wananchi. Mradi uko hatua ya ukamilishaji na utekelezaji wake unaendelea.

### 2.16.15. Mradi wa ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na ofisi 1 ya walimu shule ya msingi Kasharara

Mradi huu ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2017 ukiwa na thamani ya shilingi 47,325,000 kutokana na fedha za Mfuko wa Jimbo, Halmashauri na michango ya jamii. Mradi upo hatua ya kupiga sakafu na ukamilishaji.wake unaendelea.


**Picha 48: Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na Ofisi ya Walimu shule ya msingi Kasharara**

## 2.17. KATA YA KITWECHENKURA

Kata ya Kitwechenkura imetekeleza miradi ya maendeleo mbalimbali katika sekta za elimu, afya, maji na utawala yenye jumla ya thamani ya shilingi **419,065,000.00**. Miradi hii ambayo ipo katika hatua mbalimbali, imetekelezwa kupitia fedha Serikali Kuu, Mfuko wa Jimbo na nguvu za Wananchi. Mchanganuo wa miradi hiyo umefafanuliwa kama ifuatavyo:-

**_2.17.1._ Mradi wa ujenzi wa tanki la maji Kijiji cha Kitwechenkura**

Ujenzi wa mradi huu ulianza mnamo Agosti 2020 na ujenzi wa tanki kubwa la maji,ujenzi wa visima vidogo vidogo katika maeneo ya Kijiji cha Kitwechenkura na Rubuga unaendelea. Mradi umegharimu jumla ya kiasi cha shilingi 200,000,000 na unadhaminiwa na fedha kutoka Serikali Kuu kupitia wakala wa maji vijijini (RUWASA) .Mradi huu unatarajia kuwanufaisha wakazi wa kijiji cha Kitwechenkura wapatao 2,521



***Picha 39: Ujenzi wa tanki la maji Kitwechenkura***

**_2.17.2._ Mradi wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Msingi Kitwechenkura**

Mradi huu ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2019 na umefikia usawa wa linta, kwa gharama ya shilingi 9,365,000 fedha zitokanazo na nguvu za wananchi. Mradi huu unatarajiwa kuwanufaisha jumla ya wanafunzi 90 utakapokamilika.

**2.17.3. Mradi wa ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa Shule ya Sekondari Kitwechenkura**

Mradi huu ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2015 na umemalizika mwaka 2019 ukiwa na thamani ya shilingi 60,950,000 .Mradi huu umekamilika kutokana na fedha za Halmashauri, na nguvu za wananchi.



***Picha 40: Vyumba 4 vya madarasa vilivyokamilika Shule ya Sekondari Kitwechenkura***

**2.17.4. Mradi wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na matundu 2 ya vyoo katika mradi wa Shule ya Msingi Byailagara Kijiji cha Ruko**

Mradi huu ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2017 na unaendelea kutekelezwa ukiwa na thamani ya shilingi 27,000,000 kutokana na michango ya jamii. Utekelezaji wa miradi hii unaendelea kukamilishwa.

**2.17.5. Mradi wa ujenzi wa matundu 16 Shule ya Msingi Nyakabwera**

Ujenzi wa matundu ya vyoo hivi ulianza mnamo mwaka 2019, na bado unaendelea na tayari shimo la vyoo matundu 16 limekwishajengwa. Gharama za mradi mpaka kukamilika zinatarajiwa kuwa shilingi 23,000,000 ikiwa ni fedha zitokanazo na nguvu za wananchi.

**2.17.6. Mradi wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa, ofisi ya walimu namatundu 8 ya vyoo Shule ya Msingi Rubuga**

Mradi huu umeanza kutekelezwa mwaka 2019, na unakisiwa kugharimu shilingi 55,000,000 fedha kutoka Halmashauri na nguvu za wananchi. Mpaka sasa tayari jamvi limemwagwa na kufunga linta. Kwa ajili ya vyumba 2 na ofisi. Vilevile, matundu 8 ya vyoo yamefikia hatua ya linta Hivyo, utekelezaji wa mradi unaendelea.

**2.18.3. Ukarabati wa Kituo Cha Afya Nkwenda**

Mradi huu umekamilika, na ulitekelezwa kupitia fedha za wahisani (RBF) ambapo kiasi cha shilingi 64,000,000 zimetumika. Wanufaika wa mradi huu ni jamii ya Wana Nkwenda na maeneo jirani.

**2.18.4. Ujenzi wa matundu 8 ya vyoo vya wanafunzi Shule ya Msingi Kakerere**

Mradi huu umetumia jumla ya shilingi 6,800,000 ikiwa kiasi cha shilingi 4,000,000 ni fedha kutoka Halmashauri, na shilingi 2,800,000 ni fedha zitokanazo na nguvu za wananchi. Mradi ulianza mwaka 2018 na umekamilika.

**2.18.5. Ukarabati wa matundu 9 ya vyoo Shule ya Msingi Nyarutuntu**

Mradi huu wenye thamani ya shilingi 6,970,000 umekamilika na unatumika.Shilingi 300,000 ni fedha kutoka Halmashauri, shilingi 945,000 fedha kutoka kwa wahisani Nkwenda AMCOS na kiasi cha shilingi 2,870,000 ni fedha na michango ya wananchi.

**2.18.6. Ujenzi wa chumba 1 cha darasa Shule ya Msingi Mkapa**

Ujenzi wa mradi huu wenye thamani ya shilingi 11,470,000 kutokana na nguvu za wananchi.Jumla ya shilingi 9,400,000 zimekwishatumika.Mradi Utekelezaji wa Mradi unaendelea.

**2.18.7. Mradi wa ununuzi wa kiwanja ujenzi wa Shule ya Msingi Akanyinya**

Mradi huu wenye thamani ya shilingi 12,772,500 kwa ajili ya kununua eneo la shule pamoja na kujenga msingi kutokana na nguvu za wananchi. ujenzi umefikia hatua ya msingi wa vyumba 2 vya madarasa. Utekelezaji wa mradi unaendelea.

**2.18.8. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa shule ya sekondari Nkwenda**

Mradi huu wenye jumla ya thamani ya shilingi 34,000,000 unatekelezwa kupitia fedha za Halmashauri shilingi 3,537,500, wahisani shilingi 4,000,000 na nguvu za jamii shilingi 9,900,000.Jumla ya fedha zilizotumika mpaka sasa ni shilingi 17,437,500. Mradi uko hatua ya kuezeka na utekelezaji wake unaendelea.

**2.18.9. Ujenzi wa matundu 30 ya vyoo vya wanafunzi shule ya msingi Kaaro**

Mradi huu wenye jumla ya thamani ya shilingi 34,000,000 unatekelezwa kupitia fedha za Halmashauri shilingi 33,300,000, na nguvu za jamii shilingi 730,000.Mradi ulianza kutekelezwa mwaka 2020, umefikia hatua ya ukamilishaji na utekelezaji wake unaendelea.

**2.18.10. Mradi wa ujenzi wa matundu 12 ya vyoo shule ya msingi Mkapa**

Mradi huu wenye jumla ya thamani ya shilingi 13,000,000 unatekelezwa kupitia fedha toka Halmashauri shilingi 2,370,000, na nguvu za jamii shilingi 10,630,000.Mradi umekamilika.

**2.18.11. Ujenzi wa kisima na vioski 6 vya kutekea maji kijiji cha Nkwenda**

Mradi huu wenye thamani ya shilingi 242,000,000 unaendelea kujengwa kuanzia mwaka 2020, na unapata fedha kutoka Serikali Kuu kupitia wakala wa maji vijijini RUWASA. Tayari

kisima 1 na tepu 3 Chabataka kitongoji cha Buhanga umekamilika ukiwa umegharimu shilingi 15,000,000. Mradi utakapokamilika unatarajia kuwanufaisha wakazi wa kata ya Nkwenda na maeneo jirani.

**2.18.12. Ujenzi wa kisima kifupi cha maji Kijiji cha Nyarutuntu**

Mradi huu wenye thamani ya shilingi 5,000,000 umekamilika na unatumika. Fedha za mradi zimetokana na ufadhili wa kanisa la Anglikana. Mradi unawanufaisha wanajamii wa Kijiji cha Nyarutuntu na maeneo jirani.

**2.18.13. Ujenzi wa kisima kifupi cha maji Kijiji cha Kakerere**

Mradi huu wenye thamani ya shilingi 5,000,000 umekamilika mwaka 2020 na unatumika. Mradi umetekelezwa kwa fedha za ufadhili wa Kanisa la Anglikana. Mradi unawanufaisha wanajamii wa Kijiji cha Kakerere na maeneo jirani.

**2.18.14. Ukarabati wa Ofisi ya Kijiji Muhurile**

Mradi huu wenye thamani ya shilingi 2,100,000 ulianza kutekelezwa mwaka 2019 na bado unaendelea kutekelezwa. Fedha za utekelezaji wa mradi zimetokanana na mfuko wa jimbo kiasi cha shilingi 1,000,000, wahisani shilingi 400,000, na nguvu za Wananchi ni shilingi 400,0000.

**2.18.15. Ujenzi wa Ofisi Kijiji cha Nkwenda**

Ujenzi wa mradi huu wenye thamani ya shilingi 15,000,000 bado unaendelea kutekelezwakwa kutumia fedha kutoka mfuko wa jimbo shilingi 3,000,000, na nguvu za wananchi kiasi cha shilingi 9,000,000. Mradi kwa manufaa ya wananchi wa kijiji cha Nkwenda.

**2.18.16. Ujenzi wa Ofisi Kijiji cha Kakerere**

Mradi huu, wenye thamani ya shilingi 25,000,000 unaendelea kutekelezwa. Jumla ya matofali 17,500, mawe tripu 10 yapo eneo la mradi. Jumla ya kiasi cha shilingi 2,190,000 kimechangwa kupitia nguvu za wananchi.

**2.18.17. Mradi wa ununuzi wa kiwanja cha kujenga Ofisi ya Kijiji Runyinya**

Mradi huu wenye thamani ya shilingi 1,000,000 unaendelea na umetokana na nguvu za wananchi. Tayari wananchi wamekwisha changia jumla ya kiasi cha shilingi 500,000 na michango inaendelea.

**2.18.18. Mradi wa ujenzi wa barabara ya lami kata ya Nkwenda kupitia TARURA**

Ujenzi huu unaotekelezwa na Wakala wa Barabara vijijini (TARURA) kwa mwaka 2020, wenye thamani ya shilingi 500,000,000 umefikia 80%.TARURA inajenga barabara iendayo benki ya CRDB,na inayoshuka sokoni,stendi mpya kuelekea Eden. Fedha za mradi huu zimetoka Serikali Kuu kupitia Mfuko wa Barabara (Road Fund).

**2.18.19. Mradi wa ujenzi wa kalvati 3 na Kilomita 0.5 ya barabara kupitia TARURA**

Ujenzi huu unaotekelezwa na Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) kwa mwaka 2020, wenye thamani ya shilingi 250,000,000 umefikia 80%.TARURA inajenga barabara iendayo Benki ya CRDB na kuelekea sokoni. Fedha za mradi huu zimetoka Serikali Kuu kupitia mfuko wa barabara (Road Fund).

**2.18.20. Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kupitia TANROAD**

Wakala wa barabara nchini (TANROAD) tayari imejengwa barabara kutoka Nkwenda stendi hadi Mahakama ya Mwanzo Nkwenda kwa kiwango cha lami yenye thamani ya shilingi 387,476,500. Mradi ulianza mwaka 2020 na uko hatua ya ukamilishaji.

**2.18.21. Ujenzi wa Wodi ya Wazazi katika Kituo cha Afya Nkwenda**

Mradi wa ujenzi wa wodi ya wazazi katika Kituo cha Afya Nkwenda ulianza mwaka 2018, Jengo limeezekwa na hatua za ukamilishaji ambazo zinaendelea. Mpaka hatua ya kuezekwa mradi umetumia gharama ya Shilingi 100,000,000 kutoka fedha za Ruzuku za Serikali Kuu.



***Picha 41: Ujenzi wa Jengo la Wodi ya Wazazi Kituo cha Afya Nkwenda***

## 2.19. KATA YA ITEERA

Kata ya Iteera imetekeleza miradi ya maendeleo mbalimbali katika sekta za elimu, afya, na maji yenye jumla ya thamani ya shilingi **918,558,665.00**. Miradi hii ambayo ipo katika hatua mbalimbali, imetekelezwa kupitia fedha Halmashauri, Wahisani na nguvu za Wananchi. Mchanganuo wa miradi ni kama ifuatavyo:-

### 2.19.1. Mradi wa maji Iteera

Mradi huu, ambao ulianza kutekelezwa mwaka 2015 wenye thamani ya shilingi 655,000,000 kwa fedha toka Serikali Kuu kupitia Benki ya Dunia bado hautumiki. Mradi huu ulitarajiwa kuwahudumia wananchi wapatao 4,661 wa kata ya Iteera na maeneo jirani.



*Picha 42: Tanki la maji katika mradi mkubwa wa maji Iteera*

***2.19.2.* Mradi wa ujenzi zahanati ya Iteera**

Mradi huu wenye thamani ya shilingi 59,789,800 ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2019 kupitia fedha za Halmashauri, wahisani, na nguvu za wananchi na mradi upo katika hatua ya umaliziaji. Jengo tayari limeezekwa na kupigwa plasta nje na ndani, fremu za madirisha na milango zimepachikwa, na nilu inaendelea kupakwa ndani. Mradi huu unahita jumla ya shilingi 45,083,200 ili kulikamilisha. Endapo zahanati hii itakamilika inatarajiwa kuwahudumia wakazi wapatao 3,304 wa kata ya Iteera na vijiji jirani.



*Picha 43: Ujenzi wa jengo la Zahanati ya Iteera*

### 2.19.3. Mradi wa ujenzi zahanati ya Chanya

Mradi huu wenye thamani ya shilingi 58,277,000 ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2009 kupitia fedha za Halmashauri, wahisani, na nguvu za wananchi na mradi upo katika hatua ya umaliziaji ambapo kwa sasa umefikia 70%. Jengo tayari limeezekwa na kupigwa plasta nje na ndani. Mradi huu unahita jumla ya shilingi 62,482,200 ili kulikamilisha.Endapo zahanati hii itakamilika inatarajiwa kuwahudumia wakazi wapatao 4,260 wa kata ya Iteera na vijiji jirani.



***Picha 44: Ujenzi wa jengo la Zahanati ya Chanya***

### 2.19.4. Mradi wa utengenezaji meza 489 na madawati 489 shule ya sekondari Ntare

Mradi huu wenye thamani ya shilingi 21,925,000 ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2016 kupitia fedha za Halmashauri, na nguvu za wananchi na mradi umekamilika. Mradi umekwishawanufaisha wanafunzi wapatao 670 wa shule hii.

### 2.19.5. Mradi wa ujenzi vyumba 3 vya maabara ya sayansi sekondari ya Ntare

Ujenzi wa mradi huu ulianza mnamo mwaka 2017, na umekamilika ukiwa na thamani ya shilingi 98,066,565. Mradi umegharimiwa na fedha toka Halmashauri na nguvu za Wananchi. Mradi umewanufaisha wanafunzi 670 wa sekondari ya Ntare.



*Picha 45: Vyumba vya maabara za masomo ya Sayansi Shule ya Sekondari Ntale*

### 2.19.6. Mradi wa ukamilishaji wa ujenzi vyumba viwili vya madarasa na matundu 10 ya vyoo vya wanafunzi shule ya sekondari Ntare

Uendelezaji wa miradi hii ulianza mnamo mwaka 2018, na umekamilika kwa thamani ya shilingi 13,255,300 fedha kutoka Halmashauri, na nguvu za wananchi. Mradi huu unawahudumia wanafunzi wapatao 340 wa shule hii.



*Picha 46: Vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Ntare*

### 2.19.7. Mradi wa ujenzi matundu 11 ya vyoo vya wanafunzi shule ya Msingi Chanya

Mradi huu umeanza kutekelezwa mnamo mwaka 2017 ukiwa na thamani ya shilingi 12,245,000 kwa fedha za Jambo Bukoba na nguvu za wananchi. Mradi umekamilika na unawahudumia wanafunzi wapatao 1982 wa shule hii.

## 2.20. KATA YA MABIRA

Kata ya Mabira imetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Sekta za Elimu na Afya yenye jumla ya thamani ya shilingi **611,909,254.00**. Jumla ya miradi ishirini na mbili (22) imetekelezwa. Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali, imetekelezwa kupitia fedha Serikali

Kuu, Mfuko wa Jimbo, Wahisani na nguvu za Wananchi. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

### *2.20.*1. Mradi wa ujenzi wa nyumba nne za walimu shule ya sekondari Mabira

Mradi huu ulianza mnamo mwaka 2019 na una thamani ya shilingi 100,000,000 fedha kutoka serikali kuu kupitia Wakala wa Elimu Tanzania (TEA). Jumla ya nyumba nne za walimu zimejengwa na kukamilika.



***Picha 47: Mradi wa nyumba za Walimu Shule ya Sekondari Mabira***

### *2.20.2.* Mradi wa ujenzi wa bweni la wasichana shule ya sekondari Mabira

Mradi huu ulianza mwaka 2020 una thamani ya shilingi 68,000,000. Fedha za ujenzi wa bweni hili la wasichana zimetolewa na serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya na nguvu za Wananchi. Mradi umefikia hatua ya ukamilishaji na utekelezaji wake unaendelea.

### *2.20.3.* Mradi wa ujenzi wa bweni la wavulana shule ya sekondari Mabira

Mradi huu ulianza mwaka 2015 una thamani ya shilingi 74,000,000. Fedha za ujenzi wa bweni hili la wavulana zimetolewa na Serikali kukupitia Halmashauri ya Wilaya na nguvu za Wananchi. Mradi huu umekamilika na unatumiwa na wanafunzi 48.


*Picha 48: Bweni la Wavulana Shule ya Sekondari Mabira*

**2.20.4. Mradi wa ukarabati wa maabara za masomo ya Sayansi Shule ya Sekondari Mabira**

Mradi huu ulianza mwaka 2015 na uligahrimu kiasi cha shilingi 32,209,500 fedha kutoka Halmashauri ya Wilaya. Mradi huu umekamilika na unatumika, unahudumia jumla ya wanafunzi 692

**2.20.5. Mradi wa ujenzi wa chumba kimoja cha darasa Shule ya Sekondari Mabira**

Mradi huu ulianza mwaka 2019 una thamani ya shilingi 22,000,000. Fedha za ujenzi wa chumba hiki cha darasa zimetolewa na Halmashauri ya Wilaya na nguvu za Wananchi. Mradi umefikia hatua ya umaliziaji na utekelezaji wake unaendelea.

**2.20.6. Mradi wa ujenzi wa chumba kimoja cha darasa shule ya Sekondari Mabira**

Mradi huu ulianza mwaka 2019, una thamani ya shilingi 3,000,000. Fedha za ujenzi wa matundu 3 ya vyoo vya wavulana zimetoka Mfuko wa Jimbo. Mradi huu umefikia hatua ukamilishaji.

**2.20.7. Mradi wa ujenzi wa jengo la utawala shule ya msingi Ileega**

Mradi huu ulianza mwaka 2017 una thamani ya shilingi 69,345,254. Fedha za ujenzi wa jengo hili la utawala zimetolewa na Serikali Kuu na Halmashauri ya Wilaya .Serikali Kuu ilitoa jumla ya 50,000,000 na Halmashauri ya Wilaya ilitoa jumla ya shilingi 19,345,254. Mradi huu umekamilika na unatumika.


*Picha 49: Jengo la Utawala Shule ya Msingi Ileega*

### 2.20.8. Mradi wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi Shule Msingi Ileega na ukarabati wa madarasa

Mradi huu ulianza mwaka 2017, ulikamilika kwa gharama ya shilingi 84,722,625.00. Fedha za ujenzi wa vyumba 02 vya madarasa na ofisi zimetolewa kupitia mchango wa Halmashauri kwenye miradi ya maendeleo, Wahisani (Mfuko wa Maafa Mkoa wa Kagera) na nguvu za Wananchi. Halmashauri ilitoa jumla ya shillingi 23,192,000, Mfuko wa Maafa Mkoa wa Kagera ulitoa shilingi 59,480,625.00 na Wananchi walichangia jumla ya shilingi 2,050,000. Mradi huu umekamilika na unatumiwa na wanfunzi 96.

### 2.20.9. Mradi wa ujenzi wa matundu 10 ya vyoo Shule ya Msingi Ileega

Mradi huu ulianza mwaka 2017 una thamani ya shilingi 11,000,000.Fedha za ujenzi wa matundu haya ya vyoo zimetoka Serikali Kuu. Mradi huu umekamilika na unatumika.

### 2.20.10. Mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na matundu 2 ya vyoo Shule ya Msingi Ileega

Mradi huu ulianza mwaka 2017 na umekamilika kwa gharama ya shilingi 42,359,500. Fedha za ujenzi wa vyumba hivi viwili vya madarasa zimetoka Serikali Kuu, na matundu 2 ya vyoo yalijengwa kwa ufadhili wa Shirika la Habitat For Humanity. Mradi huu umekamilika na unatumika.

### 2.20.11. Mradi wa ujenzi wa matundu 10 ya vyoo Shule ya Msingi Nyamilima

Mradi huu ulianza mwaka 2016 una thamani ya shilingi 11,000,000.Fedha za ujenzi wa matundu haya ya vyoo zilitolewa na Serikali Kuu. Mradi huu umekamilika na unahudumia na wanafunzi 1,211.

### 2.20.12. Mradi wa ukarabati wa vyumba 12 vya madarasa na matundu ya vyoo Shule ya Msingi Nyamilima

Mradi huu ulianza mwaka 2016 uligharimu shilingi 12,200,000 ambazo zilitoka Serikali Kuu kiasi cha Shilingi 10,000,000 na Shilingi 2,200,000 zilitolewa na Shirika la Habitart For Humanity kwa ajli ya matundu 2 ya vyoo. Mradi huu umekamilika na unahudumia jumla ya wanafunzi 450 na Walimu.

### 2.20.13. Mradi wa ukamilishaji wa chumba kimoja cha darasa Shule Ya Msingi Omukagando

Mradi huu ulianza mwaka 2015 una thamani ya shilingi 12,000,000. Fedha za ukamilishaji wa chumba hiki cha darasa zilitolewa kutoka Mfuko wa Jimbo na nguvu za Wananchi. Mradi huu umekamilika na unahudumia jumla ya wanafunzi 45.

### 2.20.14. Mradi wa ujenzi wa vyoo vya walimu na wanafunzi Shule ya Msingi Omukagando

Mradi huu ulianza mwaka 2018 una thamani ya shilingi 6,725,000. Fedha za ujenzi wa matundu haya ya vyoo zimetolewa na Mfuko wa Jimbo na nguvu za Wananchi. Mradi huu umekamilika na unatumika.

**2.20.15. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na ofisi 2 za walimu Shule ya Msingi Omukagando**

Mradi huu ulianza mwaka 2016 una thamani ya shilingi 40,000,000. Fedha za ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi mbili za walimu zimetolewa na Serikali Kuu. Mradi huu umekamilika na unahudumia jumla ya wanafunzi 96 walimu 20.

**2.20.16. Mradi wa ujenzi wa chumba kimoja cha darasa Shule ya Msingi Juhudi**

Mradi huu ulianza mwaka 2020 una thamani ya shilingi 9,000,000. Fedha za ujenzi wa chumba kimoja zimetokana na michango ya Wananchi ambao wamechangia jumla ya shilingi 2,000,000. Mradi huu unaendelea na umefikia hatua ya linta

**2.20.17. Mradi wa ujenzi wa chumba cha mama na mtoto zahanati Kibimba**

Mradi huu ulianza mwaka 2020 una thamani ya shilingi 22,244,000. Fedha za ujenzi wa chumba kimoja zimetokana na michango ya Wananchi ambao wamechangia jumla ya shilingi 4,676,000. Mradi huu unaendelea na umefikia hatua ya linta utakapokamilika utahudumia jumla ya wananchi 1,345.

## 2.21. KATA YA KITWE

Kata ya Kitwe imetekeleza miradi 6 mbalimbali ya maendeleo katika Sekta za Elimu na Afya yenye jumla ya thamani ya shilingi **48,090,000.00**. Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali, imetekelezwa kupitia fedha Serikali Kuu, Mfuko wa Jimbo, Wahisani na nguvu za Wananchi. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

***2.21.1.*** **Mradi wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Chitwe**

Mradi huu ulianza mwaka 2015, umejengwa kwa gharama ya Shilingi 30,210,000. Fedha za ujenzi wa chumba kimoja zimechangwa na Wananchi, Halmashauri, Mfuko wa Jimbo na Serikali Kuu ambapo wananchi wamechangia shilingi 2,000,000, Mfuko wa Jimbo Shilingi 3,000,000, Halmashauri 210,000 na Serikali Kuu 25,000,000. Mradi huu umekamilika na unatumika unahudumia wanafunzi 80.



***Picha 50: Vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Chitwe***

**2.21.2. Mradi wa ukamilishaji wa ujenzi wa matundu 12 ya vyoo Shule ya Msingi Chitwe**

Mradi huu ulianza mwaka 2016, umekamilishwa kwa gharama ya Shilingi 4,300,000. Fedha za ujenzi wa matundu 12 vya vyoo zimechangwa na Wananchi. Mradi huu umekamilika na unatumika unahudumia wanafunzi 300.

**2.21.3. Mradi wa ukarabati wa vyumba 5 vya madarasa Shule ya Msingi Chitwe**

Ukarabati wa madarasa ulianza mwaka 2017 kwa gharama ya Shilingi 1,846,000 kwa nguvu ya Wananchi na mchango wa Halmashauri. Mradi huu umekamilika na unatumika unahudumia wanafunzi 200.

**2.21.4. Uendelezaji wa chumba cha darasa na Ofisi ya walimu Shule ya Msingi Ibamba**

Mradi huu ulianza mwaka 2016 kwa gharama ya Shilingi 1,434,000 kwa nguvu za Wananchi. Mradi huu bado unaendelea utakapokamilika utahudumia wanafunzi 45 na walimu 18.

**2.21.5. Ukamilishaji wa chumba 1 cha darasa Shule ya Msingi Nyerere**

Ukamilishaji ulianza mwaka 2016 una thamani ya shillingi 3,100,000 kwa fedha za Mfuko wa Jimbo na nguvu ya Wananchi ambapo mfuko wa jimbo ulitoa shilingi 2,000,000 na Wananchi walichangia shilingi 1,100,000. Mradi huu umekamilika na unatumika unahudumia wanafunzi 45.

**2.21.6. Ukamilishaji wa Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Kitwe**

Ukamilishaji wa ujenzi wa Zahanati ulianza mwaka 2019 kwa gharama ya Shilingi 7,200,000 ikiwa ni nguvu ya Wananchi katika kukamilisha ujenzi wa Zahanati hiyo ili iweze kutumika. Mradi huu umekamilika na unatumika unahudumia 1,256.

## 2.22. KATA YA KAMULI

Kata ya Kamuli imetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Sekta za Elimu na Afya yenye jumla ya thamani ya shilingi **539,499,438.00**. Jumla ya miradi saba (7) imetekelezwa. Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali na imetekelezwa kupitia fedha Serikali Kuu, Mfuko wa Jimbo, Wahisani na nguvu za Wananchi. Mchanganuo wa miradi ni kama ifuatavyo:-

***2.22.1.* Mradi wa ujenzi wa chumba cha darasa Shule ya Sekondari Kamuli**

Mradi huu ulianza mwaka 2019, una thamani ya shilingi 14,637,795.00. Fedha za ujenzi wa chumba kimoja cha darasa zimetokana na mchango wa Halmashauri na Serikali Kuu, ambapo Serikali Kuu wamechangia Shilingi 13,188,795, Halmashauri wamechangia Shilingi 1,449,000. Mradi huu umekamilika na unahudumia wanafunzi 40.



*Picha 51: Chumba cha darasa Shule ya Sekondari Kamuli*

**2.22.2. Mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya Kituo cha Afya Kamuli**

Mradi huu ulianza mwaka 2018 kwa kujenga jumla ya majengo 4 kwa gharama ya Shilingi 479,306,940. Fedha za uboreshaji wa miundombinu ya kituo cha afya zimetoka Serikali Kuu, Mfuko wa Afya na nguvu ya Wananchi ambapo Serikali Kuu imetoa Shilingi 400,000,000, Mfuko wa Afya umechangia Shilingi 75,113,740 na Wananchi wamechangia Shilingi 4,193,200. Mradi huu umekamilika na unahudumia wananchi wapatao 17,205 wa Kata ya Kamuli na maeneo jirani.



*Picha 52: Wodi ya Wazazi Kituo cha Afya Kamuli*

**2.22.3. Mradi wa ujenzi wa matundu 11 ya vyoo shule ya msingi Kamuli**

Mradi huu ulianza mwaka 2019 una thamani ya shilingi 14,637,795 ambazo zimetokana na fedha za Halmashauri na michango ya wananchi. Mradi umekamilika na unatumika.

**2.22.4. Mradi wa ujenzi wa matundu 8 ya vyoo shule ya msingi Rwabigaga**

Mradi una thamani ya shilingi 6,417,500, fedha kutoka Halmashauri ya Wilaya pamoja na wananchi, Mradi ulianza mwaka 2017, umekamilika na unatumika.

**2.22.5. Mradi wa ujenzi wa matundu 8 ya choo shule ya msingi Msisha**

Mradi una thamani ya shilingi 3,499,408.00, fedha za Mfuko wa Jimbo pamoja na wananchi Mradi ulianza mwaka 2019, umekamilika na unatumika.

**2.22.6. Mradi wa ujenzi wa jengo la kutolea huduma za mkoba**

Mradi unakisiwa kugharimu Shilingi 13,000,000 Jumla ya Shilingi 2,855,000 kutoka Halmashauri na nguvu za Wananchi zimekwishatumika kutekeleza mradi huu. Mradi ulianza mwaka 2019 na ukamilishaji unaendelea.

**2.22.7. Uwekezaji katika Msitu wa Mtagata wa Rwabigaga**

Serikali imewekeza Shilingi 8,000,000.00 katika msitu huo kwa ajili ya shughuli za kuchora ramani ya Msitu, Kutambua mipaka na kusimika bikoni, kubaini rasilimali zilizoko katika msitu ikiwemo wanyama, ndege na miti, chanzo cha maji kitakachonufaisha Wananchi wa Rwabigaga pamoja na mpango wa usimamizi wa sheria ndogo ndogo.

## 2.23. KATA YA BUGARA

Kata ya Bugara imetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Sekta za Elimu na Afya yenye jumla ya thamani ya shilingi **81,584,500.00**. Jumla ya miradi 12 imetekelezwa. Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali, imetekelezwa kupitia fedha Serikali Kuu, Mfuko wa Jimbo, Wahisani na nguvu za Wananchi kama inavyofafanuliwa hapa chini.

**2.23.1. Mradi wa ujenzi wa ofisi ya kata Bugara**

Mradi huu ulianza mwaka 2018 unakisiwa kukamilika kwa gharama ya Shilingi 18,278,000. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha zinazochangwa na Wananchi na nguvu zao. Mradi huu bado unaendelea hatua za ukamilishaji.

**2.23.2. Mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Kijiji Bugara**

Mradi huu ulianza mwaka 2017 unakisiwa kukamilika kwa gharama ya Shilingi 18,200,000. Jengo hili la ofisi linajengwa kwa nguvu za Wananchi. Mradi uko hatua ya uezekaji na utekelezaji wake unaendelea.

**2.23.3. Mradi wa ujenzi wa ofisi ya Kijiji Rwakabunda**

Mradi huu ulianza mwaka 2019 umetumia gharama ya shilingi 8,500,000. Fedha za ujenzi wa jengo la Ofisi ya Kijiji zimetokana na nguvu za wananchi. Utekelezaji wa mradi huu unaendelea.

**2.23.4. Mradi wa ujenzi wa matundu 10 ya vyoo vya wanafunzi Shule ya Msingi Rwakabunda**

Mradi huu ulianza mwaka 2019 na umetumia gharama ya shilingi 12,000,000. Fedha za ujenzi wa vyoo zimetokana na Mfuko wa Jimbo na nguvu za Wananchi. Mradi huu bado unaendelea na unatarajia kuhudumia wanafunzi 615 baada ya kukamilika.

**2.23.5. Mradi wa ukamilishaji wa nyumba 1 ya mwalimu shule ya Msingi Mugaba**

Mradi umetumia gharama ya Shilingi 6,162,000.00, fedha za Mfuko wa Jimbo pamoja na nguvu za Wananchi. Mradi ulianza mwaka 2019 na utekelezaji wake unaendelea.

**2.23.6. Mradi wa ujenzi wa choo cha walimu shule ya msingi Bugara**

Mradi una thamani ya Shilingi 1,450,000.00, fedha zilizotokana na nguvu za Wananchi. Mradi ulianza mwaka 2019, umekamilika na unatumika.

**2.23.7. Mradi wa ujenzi wa bafu za watumishi na wagonjwa zahanati ya Bugara**

Mradi huu umegharimu Shilingi 2,994,500.00 fedha kutoka Serikali Kuu (RBF) pamoja na nguvu za Wananchi. Mradi ulianza mwaka 2020, umekamilika na unatumika.

**2.23.8. Ukamilishaji wa majengo Zahanati ya Bugara**

Mradi huu ulianza mwaka 2016 na kutumia gharama ya Shilingi 2,000,000, fedha za Mfuko wa Jimbo na nguvu za Wananchi. Mradi huu umekamilika na unahudumia zaidi ya Wananchi 9,313.

**2.23.9. Ujenzi wa kisima cha maji Zahanati ya Bugara**

Mradi huu ulianza mwaka 2017 kwa gharama ya Shilingi 3,500,000, Fedha zilizotokana na nguvu ya Wananchi. Mradi huu umekamilika na unahudumia Wananchi.

**2.23.10. Ukamilishaji wa matundu 2 ya vyoo Zahanati ya Bugara**

Mradi huu ulianza mwaka 2017 kwa gharama ya Shilingi 2,500,000, fedha zilizotokana na nguvu ya Wananchi. Mradi huu umekamilika na unatoa huduma.

**2.23.11. Mradi wa ujenzi wa matundu 10 ya vyoo shule ya msingi Bugara**

Mradi huu ulianza mwaka 2018, umekamilishwa kwa gharama ya Shilingi 6,000,000 ikiwa ni nguvu za Wananchi. Mradi huu umekamilika na unahudumia zaidi ya watu 876.

**2.24.12. Mradi wa ujenzi wa vyumba 6 vya madarasa Shule ya Sekondari Bugara**

Mradi huu ulianza mwaka 2018, mradi huu umegharimu kiasi cha Shilingi 64,000,000 kufikia hatua ya kuezekwa. Fedha za ujenzi wa vyumba 6 vya madarasa shule ya sekondari zimetokana mchango wa Halmashauri na nguvu za Wananchi. Mradi huu bado unaendelea na utekelezaji.

## 2.24. KATA YA BUSINDE

Kata ya Businde imetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Sekta za Elimu, Afya na Utawala yenye thamani ya Shilingi **315,037,522.00**. Fedha hizo zimetumika kutekeleza jumla ya miradi 10. Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali, imetekelezwa kupitia fedha za Serikali Kuu, Halmashauri, Mfuko wa Jimbo, Wahisani na nguvu za Wananchi. Mchanganuo wa miradi umefafanuliwa kama ifuatavyo:-

***2.24.1.*** **Mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Kata Businde**

Mradi huu ulianza mwaka 2012 na mpaka hatua ulipofikia jumla ya Shilingi 25,000,000 zimetumika. Fedha za ujenzi wa ofisi ya kata zimetolewa na Halmashauri na nguvu za Wananchi. Mradi huu bado unaendelea kukamilishwa.



***Picha 53: Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Kata ya Businde***

***2.24.2.*** **Ujenzi wa chumba 1 cha darasa Shule ya Msingi Omunchwekano**

Mradi huu ulianza mwaka 2019, umetekelezwa kwa gharama ya shilingi 14,212,522, Fedha za ujenzi wa chumba cha darasa zimetolewa na Serikali Kuu kupitia mfuko wa malipo kutokana na matokeo (P4R) pamoja na michango ya Wananchi ambapo Serikali Kuu (P4R) imechangia shilingi 9,275,522 na Wananchi wamechangia Shilingi 4,937,000. Mradi huu umekamilika na unahudumia wanafunzi 45.

**2.24.3. Mradi wa ujenzi wa chumba 1 cha darasa Shule ya Msingi Maendeleo**

Mradi huu ulianza mwaka 2019, umegharimu shilingi 20,000,000, Fedha za ujenzi wa chumba cha darasa zimetolewa na Serikali Kuu (P4R) na nguvu za Wananchi ambapo Serikali (P4R) imetoa Shilingi 15,097,133.40 na Wananchi wamechangia Shilingi 4,902,867.60. Mradi huu umekamilika na unahudumia wanafunzi 45.

**2.24.4. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Businde**

Mradi huu ulianza mwaka 2019, mpaka hatua ya umaliziaji umetumia gharama ya Shilingi 41,785,000 kupitia mchango wa Halmashauri na nguvu ya Wananchi. Mradi huu bado unaendelea kutekelezwa.

**2.24.5. Mradi wa ujenzi wa chumba 1 cha darasa Shule ya Msingi Rubale**

Mradi huu ulianza mwaka 2019, umetumia gharama ya Silingi 7,000,000 ikiwa ni fedha za ufadhili wa Jambo Bukoba (4,000,000) na michango ya Wananchi (3,000,000). Mradi huu bado unaendelea na umefikia hatua ya uezekaji.

**2.24.6. Ujenzi wa chumba 1 cha darasa Shule ya Msingi Omunchwekano**

Mradi huu ulianza mwaka 2013, umekadiriwa kugharimu kiasi cha Shilingi 15,840,000. Mpaka ulipofikia umetumia jumla ya Shilingi 9,000,000. Fedha za ujenzi wa chumba cha darasa zimetolewa kwa ufadhili wa Jambo Bukoba na nguvu ya Wananchi ambapo wahisani (JAMBO BUKOBA) wamechangia shilingi 4,000,000 na wananchi wamechangia shilingi 5,000,000. Mradi huu bado unaendelea na jengo limeezekwa na hatua za ukamilishaji zinaendelea.

**2.24.7. Mradi wa ujenzi wa chumba 1 cha darasa Shule ya Msingi Maendeleo**

Mradi huu ulianza mwaka 2017 umegharimu jumla ya Shilingi 7,200,000 zilizotokana na nguvu ya Wananchi. Mradi huu bado unaendelea na jengo lipo usawa wa madirisha.

**2.24.8. Mradi wa ujenzi wa Zahanati Kijiji Nyakashenyi**

Mradi huu ulianza mwaka 2009 na umegharimu jumla ya Shilingi 38,000,000, fedha kutokana na mchango wa Halmashauri na nguvu ya Wananchi. Mradi huu unaendelea na jengo lipo usawa wa madirisha.

**2.24.9. Mradi wa ujenzi wa nyumba 1 ya Mganga Zahanati ya Nyakashenyi**

Mradi huu ulikisiwa kukamilika kwa gharama ya Shilingi 46,000,000 na mpaka usawa wa linta kiasi cha Shilingi 6,200,000 kimetumika ikiwa ni fedha kutokana na michango ya Wananchi. Mradi huu majengo yake yamekamilika, hatua za usajili zinafanyika ili zahanati ianze kutoa huduma.

**2.24.10. Mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Kijiji Omunchwekano**

Mradi huu ulianza mwaka 2019 na unakisiwa kukamilika kwa Shilingi 100,000,000.00. Hadi kufikia hatua ya kukamilisha msingi, jumla ya Shilingi 6,245,000 kutokana na nguvu za Wananchi zimetumika. Mradi huu bado unaendelea.



*Picha 54: Baadhi ya majengo ya zahanati ya Kijiji Nyakashenyi*

## YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI ... - 1 -

1.1. MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA ILANI KWA KILA SEKTA ... - 1 -

1.2. HITIMISHO ... - 3 -

2.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI MBALIMBALI KIKATA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2015-2020 ... - 3 -

2.1. KATA YA RUTUNGURU ... - 3 -

2.2. KATA YA KIBINGO ... - 1 -

2.3. KATA YA MURONGO ... - 2 -

2.4. KATA YA BUGOMORA ... - 6 -

2.5. KATA YA KIBARE ... - 7 -

2.6. KATA YA KYERWA ... - 9 -

2.7. KATA RUKURAIJO ... - 5 -

2.8. KATA ISINGIRO ... - 9 -

2.9. KATA KAISHO ... - 12 -

2.10. KATA NYARUZUMBURA ... - 15 -

2.11. KATA KIKUKURU. ... - 16 -

2.12. KATA YA NYAKATUNTU ... - 18 -

2.13. KATA YA KAKANJA ... - 19 -

2.14. KATA YA KIMULI ... - 21 -

2.15. KATA YA RWABWERE ... - 22 -

2.16. KATA YA SONGAMBELE ... - 24 -

2.17. KATA YA KITWECHENKURA ... - 27 -

2.18. KATA YA NKWENDA ... - 1 -